
'SWAHILI FASHION WEEK 2020'

## Inathaminisha mavazi halisi ya Kiafrika



UKURASA 13

## Barcelona kumweka Messi njia panda




UKURASA 22


MAISHA

NOVEMBA 8, 2020 Nipashe — Baba, Mama na Mwana — *Jumapili*



Ukurasa 14

**Kula nyanya chungu upate faida kiafya**



Ukurasa 15

**MAISHA NI NYUMBA**

Athari udongo wa mfinyanzi katika ujenzi wa nyumba



**HARUSI**

Ukurasa 12


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Novemba 8, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0580393

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




'CONCEALER'

**Kipodozi kinachompa ujana mwanamke**

Ukurasa 14

RIPOTI MAALUM

# Barabara zinavyomaliza hazina ya wanyamapori

• **Kila** siku wanahesabu 'misiba', CAG afukua ushuhuda mpya... *Endelea ukurasa 4*

## YALIYOMO


UKURASA WA 2

**VIONGOZI DINI WATAKA WALIOSHINDWA UCHAGUZI MKUU WAKUBALI YAISHE**

UKURASA WA 3

**MUUGUZI MATATANI KWA TUHUMA WIZI VIFAA TIBA**




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Debora Magiligimba, akionyesha vifaa tiba kwa waandishi wa habari mkoani humo jana, vilivyoibwa katika Hospitali ya Rufani ya mkoa huo. **Habari zaidi Uk. 3. PICHA: MARCO MADUHU**

## Trump atangaza kutokubali matokeo



UKURASA 17





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play

Download on the App Store




## Bunge la 12 kuanza kwa staili ya kipekee

UKURASA 2

MICHEZO **NDAYIRAGIJE ATAMBA KUWASHANGAZA** UK.23

**MAONI, KATUNI** UK.6

## ...Uchaguzi Spika wa Baraza la Wawakilishi kuanza leo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUTANO wa mwanzo wa Baraza la 10 la Wawakilishi unatarajiwa kuanza rasmi leo ukitarajiwa kuwapo na shughuli mbalimbali, ukiwamo uchaguzi wa spika wake.

Akizungumza na waandishi wa habari visiwani hapa jana, Katibu wa Baraza la Wawakilishi, Raya Mselem, alisema uchaguzi wa spika wa baraza hilo utafayika leo.

Alisema waliochukua fomu ya kugombea nafasi hiyo ni watano akiwamo aliyekuwa Spika wa Baraza hilo, Zuberi Ali Maulid, kutoka Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Aliwataja wengine kuwa ni Ali Makame kutoka Chama cha Wananchi (CUF), Naima Salum Hamad kutoka chama cha UDP, Hamad Mohamed Ibrahim (UPDP) na Ameri Hassan Ameri kutoka Chama cha Demokrasia Makini.

Katibu huyo alisema baada ya uchaguzi huo, kutakuwa na kiapo cha Spika na kufuatiwa na kiapo cha uaminifu kwa wajumbe wa baraza hilo.

Alisema pia kutakuwa na uchaguzi wa naibu spika wa baraza hilo na kufuatiwa na uzinduzi wa baraza la 10. Alisema Novemba 11 mwaka huu, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, atalifungua rasmi baraza hilo. Katibu huyo alisema tayari wajumbe wa majimbo 50 ya uchaguzi ya Zanzibar walitangazwa na Tume ya Uchahuzi Zanzibar wameshapewa taarifa kuhusu shughuli hiyo ambao ni kutoka vyama vya CCM na ACT-Wazalendo.

"Chama cha Mapinduzi tayari wameshajibu barua tuliyowapelekea kuhusu wajumbe wa baraza la wawakilishi kutokea chama hicho kuhudhuria vikao, lakini ACT hadi sasa bado hawajajibu barua yetu kuhusu ushiriki wa wajumbe wa baraza walitangazwa na tume," alisema. Hata hivyo, alisema wameshapokea wajumbe wa baraza la wawakilishi wa viti maalum kutoka CCM pekee ambao ni 18.

Katibu huyo aliwataka wananchi kuendelea kufuatilia shughuli mbalimbali za chombo hicho.



Katibu wa Bunge, Stephen Kagaigai, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma jana, kuhusu mkutano wa kwanza wa Bunge la 12, unaotarajiwa kuanza Jumanne ijayo. Kulia ni Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa wa Ofisi ya Bunge, Daniel Eliufoo. **PICHA: BUNGE**

# Safari Bunge la 12 rasmi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKUTANO wa kwanza wa Bunge la 12, unatarajiwa kuanza Novemba 10 mwaka huu huku majukumu sita yakitajwa kufanyika ndani ya siku nne tu ikiwamo uchaguzi wa spika na kuthibitisha jina la Waziri Mkuu.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Katibu wa Bunge, Stephen Kagaigai, alisema kikao hicho kimeitishwa baada ya Tangazo la Rais lililotolewa Novemba 5 mwaka huu kwenye Gazeti la Serikali toleo maalum namba 942A.

Pia, alisema utaratibu huo unafuatia tangazo alilolitoa kwenye gazeti hilo hilo toleo maalum namba 1763A na 1764A Novemba 5, mwaka huu kuhusu kuwa wazi kwa nafasi ya spika na naibu spika pamoja na kanuni za uchaguzi wa viongozi hao.

"Wabunge wote wanafahamishwa kwamba shughuli za usajili na taratibu zingine za kiutawala zitafanyika Ofisi ya Bunge Dodoma kuanzia tarehe 7-9, Novemba mwaka huu, hivyo kikao cha kwanza cha mkutano wa kwanza wa Bunge kitafanyika Novemba 10, mwaka huu kama ilivyotamkwa kwenye Tangazo la Rais," alisema.

Alitaja shughuli zitakazofanyika kuwa ni kusomwa kwa tangazo la Rais kuitisha Bunge, uchaguzi wa spika, kiapo cha uaminifu kwa wabunge wote, kuthibitisha jina la Waziri Mkuu, uchaguzi wa naibu spika na ufunguzi rasmi wa bunge jipya utakaofanywa na Rais Dk. John Magufuli.

Vilevile, aliwasisitiza wabunge wateule wote kufika wakiwa na nyaraka mbalimbali ikiwamo hati ya kuchaguliwa au kuteuliwa kuwa mbunge, nakala ya kitambulisho cha taifa, kadi ya benki yenye namba ya akaunti ya mbunge na cheti cha ndoa kinachotambuliwa na serikali kwa wenye ndoa.

"Nyaraka zingine ni cheti cha kuzaliwa cha watoto wenye umri chini ya miaka 18 kwa wenye watoto, vyeti vya elimu au taaluma, picha nakala nane na nakala ya wasifu wa mbunge," alisema.

Alifafanua kuwa nakala ya wasifu wa mbunge ni muhimu kwa kuwa wanaitumia wakati wa kupanga wajumbe wa kamati za kudumu za Bunge.

Alipoulizwa kuhusu kuhitimishwa kwa Bunge, katibu huyo alisema shughuli hizo zinatarajiwa kuhitimishwa Ijumaa Novemba 13, mwaka huu.

Uzoefu unaonyesha mkutano huo wa kwanza wa Bunge umekuwa ukifanyika kwa wiki mbili, lakini safari hii muda unaonekana kupunguzwa.

# Viongozi wa dini watoa neno walioshindwa uchaguzi mkuu

**Na Romana Mallya**

VIONGOZI wa dini kutoka Tanzania Bara na Zanzibar, wamewataka wanasiasa walioshindwa katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu, kukubali matokeo kwa sababu Mungu ametaka iwe hivyo.

Wakizungumza jana katika kongamano la kumshukuru Mungu baada ya uchaguzi lililobebwa na kaulimbiu ya 'Amani yetu, Maendeleo Yetu', viongozi hao walisema walioshindwa wakihitaji ushauri kwao, milango iko wazi.

Askofu wa Kanisa la Full Gospel Bible Fellowship (FGBF), Zacharia Kakobe, alikumbusha kuwa katika Katiba ya nchi Ibara ya 41(7), iwapo mgombea ametangazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwamba amechaguliwa kuwa Rais, hakuna mahakama yoyote itakayokuwa na mamlaka ya kuchunguza kuchaguliwa kwake.

"Maana yake ni kwamba shughuli yote imeshafungwa na wagombea wote katika kusaini maadili, yalijengwa na Katiba.

"Hakuna mamlaka nyingine ya kuchunguza kuhusu kuchanguliwa Rais, labda kwa wakati mwingine kama katiba itabadilishwa," alisema.

Askofu Kakobe alisema licha ya baadhi ya wagombea kuwataka wananchi kujitokeza barabarani baada ya uchaguzi, hakuna aliyefanya hivyo kwa sababu watu wameafiki kuwa mchakato huo umekwisha.

"Wananchi safari hii wamekuwa kama wajumbe, kimya kimya wametoa ujumbe kuwa uchaguzi umekwisha ndiyo maana wamekataa kujitokeza barabarani. Uvunjwe mguu au mkono halafu huyo aliyekuhamasisha kesho unamwona ameunga mkono juhudi," alisema.

Aliwataka wanasiasa wahitimishe vijembe na waliotangazwa kushinda wawapende waliotangazwa kushindwa kwa kuwa bila kutangazwa aliyeshindwa, wasingetangazwa kushinda.

"Ni muhimu kuzingatia tuliotangazwa kushindwa kwamba kwa mshindani yeyote ni mwiko kukata tamaa, usikate tamaa na kuona ndiyo mwisho wa mambo yote, bado yapo matumaini," alisema.

Askofu Mkuu wa WAPO Mission International, Sylvester Gamanywa, alisema hakuna mamlaka inayokuwapo isiporuhusiwa na Mungu.

"Matokeo haya kwa pande zote yameshtua wengi na wapo ambao mioyo yao inaumia kwa sababu mbalimbali, nasaha zetu ni kuganga mioyo na kukubali matokeo kwa hiari kwa sababu ndivyo Mungu alivyotaka na kama kutahitajika ushauri, viongozi wa dini wapo," alisema.

Katibu wa Mufti wa Zanzibar, Sheikh Khalid Ali Mfaume, katika mada yake iliyokuwa ikizungumzia 'Amani Msingi wa Maendeleo', alisema ili uchumi uendelee, ni lazima kusitokee uharibifu wowote katika ardhi na kuhatarisha amani.

"Kama kuna jambo lolote ama mgogoro wowote, ni vizuri tukae meza moja kuzungumza ili amani iendelee kuwapo," alisema.

Mjumbe wa Masheikh Mkoa wa Dar es Salaam, Yusufu Diwani, aliyemwakilisha Sheikh wa Mkoa wa Dar es Salaam, alisema kinachotakiwa ni kulinda amani.

Askofu wa Kanisa la Anglicana kutoka Zanzibar, Dk. Michael Hafidh, alisema visiwani huko wamekuwa na amani ya kutosha.

"Tunamwomba Rais asiwe na hofu wala woga tumeshamaliza uchaguzi, wengine wakiturudisha nyuma ni wao, sisi tunakwenda mbele, uchaguzi ulikuwa wa amani, tunamwomba Rais, baraza atakalolichagua, alichague kwa kufanya kazi, kazi yetu ni kumwombea," alisema.

Askofu Charles Salala wa AICT Dayosisi ya Pwani, katika mada yake ya kupokea matokeo kwa amani, alisema neno hekima limebeba maana ya uwezo wa akili aliyonayo mtu kuongoza na kutoa uamuzi ulio sahihi.

Alisema kila nchi ina matatizo yake na watu wake ndiyo wanaotakiwa kuyamaliza, hivyo sera ya kuyamaliza kwa kutumia taifa lingine haoni kama ni sawa.

Katibu wa Jumuiya ya Isimailia, Mahabubu Kasimu, alisema duniani kuna watu wanaiangalia Tanzania kwa furaha, wivu na wengine kuchokonoa na kuleta uchochezi.

"Watanzania tuache ushabiki, vijembe mitandaoni, tushikamane na viongozi wetu ili maendeleo yaje kwa kasi kama tunavyoyahitaji," alisema.

# TAKUKURU Ruvuma yaokoa mamilioni

**Na Gideon Mwakanosya,**
SONGEA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Ruvuma, imeokoa Sh. 107,478,845 (milioni 107) katika robo ya kwanza ya mwaka huu wa bajeti kutokana na uchunguzi mbalimbali uliofanya.

Mkuu wa taasisi hiyo Mkoa wa Ruvuma, Hamza Mwenda, alisema juzi kuwa katika kutimiza majukumu yake, taasisi hiyo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali walifanikiwa kuokoa kiasi hicho cha fedha.

Mwenda alibainisha kuwa Sh. 488,000 zimepatikana kutokana na marejesho ya madeni ya Benki ya Wananchi Mbinga (MCB), fedha ambazo ziliwekwa kwenye akaunti ya Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU iliyoko Benki Kuu.

Alisema Sh. 94,420,845 (milioni 94) zimeokolewa kutokana na uchunguzi unaoendelea katika vyama vya kuweka na kukopa(SACCOS) wilayani Songea na Sh. 1,436,000 (milioni 1.436) ni marejesho ya madeni ya Muungano SACCOS ya wilayani Namtumbo.

Alisema Sh. 2,465,000 (milioni 2.465) ni marejesho ya madeni ya Mbinga Teachers SACCOS na Sh. 1,779,000 (milioni 1.779) ni marejesho ya madeni ya Mbinga Kurugenzi SACCOS ambapo fedha zote za SACCOS ziliwekwa kwenye akaunti za vyama husika.

Alifafanua kuwa Sh. milioni 5.89 ni fedha zilizookolewa wilayani Nyasa kwenye deni feki alilowekewa Ufunuo Chirwa na Taasisi ya Maboto, akifafanua kuwa mkopaji alistahili kulipa Sh. milioni nne lakini aliwekewa deni la Sh. milioni 9.89 kwa njia za ujanja ujanja.

Mkuu huyo alitoa wito kwa wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa TAKUKURU katika mapambano dhidi ya kupinga rushwa kwa kukemea na kuzuia vitendo vyote vyenye viashiria ya rushwa katika jamii na kwenye ofisi za umma.

# Wajitokeza kupima saratani, tezi dume

**Na Richard Makore,**
MWANZA

ZAIDI ya wananchi 300 katika mikoa mbalimbali ya Kanda ya Ziwa, wamejitokeza kupima afya zao bure katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Bugando ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Mionzi Duniani.

Wananchi hao wametumia siku mbili, juzi na jana kufika, hospitalini hapo kwa ajili ya kupima homa ya ini, saratani, tezi dume kwa wanaume na kansa ya shingo ya kizazi kwa wanawake.

Daktari Bingwa wa Mionzi katika Hospitali hiyo, Magreth Magambo, akizungumza wakati wa upimaji huo, alisema wamepokea watu kutoka mikoa mbalimbali ya Kanda ya Ziwa kwa ajili ya kupata huduma hiyo.

Kutokana na hali ilivyojitokeza katika upimaji huo, Dk. Magambo alisema kuna haja huduma hiyo kusogezwa hadi ngazi ya wilaya ili kutoa fursa kwa wananchi wengi.

Dk. Magambo aliongeza kuwa baadhi ya magonjwa waliyokutwa nayo ni pamoja na tezi dume, kansa ya kizazi na homa ya ini.

Watalaam wa afya wanasema asilimia 40 ya wagonjwa wa kansa wanatoka mikoa ya Kanda ya Ziwa kutokana na madini mbalimbali yanayopatikana katika eneo hilo.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi jijini Mwanza, Ofisa Mionzi kutoka Hospitali ya Rufani ya Bugando, Dk. Evance Nabugare, alisema madini mbalimbali yakiwamo dhahabu na almasi yanachangia kuwapo ugonjwa huo.

Hatua hiyo, alisema imesababisha wajipange kuadhimisha Siku ya Mionzi Duniani ambayo hufanyika Novemba 8 kila mwaka.

Pamoja na asilimia kubwa ya wagonjwa kutoka katika mikoa hiyo, alibainisha kuwa saratani ya kibofu ndiyo inayoongoza. Ugonjwa mwingine ambao ni tishio kwa mikoa hiyo, kwa mujibu wa mtaalamu huyo, ni kicho.

Dk. Nabugare alisema katika kuadhimisha Siku ya Mionzi Duniani, wanatoa huduma za upimaji bure ikiwamo kipimo cha MRI na kwamba kati ya watu 10 wanaowapima, watu watatu wanakutwa na kansa.

Aliongeza kuwa ugonjwa wa kansa mgojwa akiwahi katika hatua ya mwanzo anapona lakini wagonjwa wengi wanafika hospitali wakiwa katika hatua mbaya.

Dk. Nabugare alisema mwaka 1895, mgunduzi wa mionzi, aligundua kipimo cha mionzi na kwamba katika kipindi chote hicho, watalaam mbalimbali na wananchi duniani wamekuwa wakiadhimisha siku huyo.




Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Abubakar Kunenge (wa pili kushoto), akiongoza matembezi ya amani wakati wa uzinduzi wa maadhimisho ya wiki ya kuzuia na kudhibiti magonjwa yasiyoambukiza jijini humo jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Muuguzi mbaroni tuhuma wizi vifaa tiba

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

MUUGUZI wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga, Madaraka Joseph (32), anashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kuiba vifaa tiba.

Kamanda wa Polisi Mkoani Shinyanga, Debora Magiligimba, akitoa taarifa hiyo jana kwa vyombo vya habari, alisema muuguzi huyo baada ya kuiba vifaa hivyo, aliviuza kwa mmiliki wa Zahanati ya Suka Wazazi, Suka Charles, iliyoko wilayani Kahama ambaye naye anashikiliwa.

Alisema tukio hilo lilitokea Oktoba 13, mwaka huu, majira ya saa 10:00 jioni. Alisema muuguzi huyo aliiba mashine mbili za kuangalia wagonjwa katika chumba cha upasuaji, aina ya Edan Im8 na Data SCOP 1 zenye thamani ya Sh. milioni 26.

Magiligimba alisema baada ya kufanya uchunguzi, polisi walibaini kuwa vifaa tiba hivyo viliuzwa kwa Charles kwa makubaliano ya Sh. milioni nne alikuwa ameshatanguliziwa Sh. milioni mbili.

"Jeshi la Polisi tulifanya upekuzi nyumbani wa Suka Charles na kufanikiwa kupata mashine zote pamoja na vifaa vyake, ambavyo ni 'Patient monitor' mbili, BP Machine Accessories, Cable Wires na Medical Molecular," alisema Magiligimba.

Alitaja vifaa vingine kuwa ni Oxygen Concentrator moja yenye namba 598 na Oxygen Concentrator Intesty yenye namba 601.1/1EC/601-1 na kubainisha kuwa watuhumiwa wote watafikishwa mahakamani upelelezi utakapokamilika.

Pia Kamanda alitoa wito kwa watumishi wa umma kuacha kujihusisha na wizi wa mali za umma ambazo zinasababisha wananchi kukosa huduma na kuibebesha lawama serikali kuwa haitoi huduma stahiki za afya kwa wananchi wake.

RIPOTI MAALUM

# Barabara zinavyomaliza hazina ya wanyamapori

**Na Sanula Athanas**

NI barabara ya lami, kipande cha kilomita 50 ndani ya mandhari wanayoishi wanyamapori, ambayo upitaji wa magari unaibebesha serikali hasara kuu tatu, kiwango cha kuitoa machozi.

Serikali kupitia chombo chake, Wizara ya Maliasili na Utalii, inalalamika kwamba katika kila saa 24, ajali hizo zinasababisha kifo siyo chini ya mnyama mmoja kwenye Hifadhi ya Taifa Mikumi (MINAPA) inakopita barabara hiyo.

Malalamiko hayo yanaenda mbali kwa kugusa pia athari mbaya za kimazingira zinazokinzana na mahitaji ya ustawi wa hifadhi, wakati huo huo MINAPA inabeba mzigo mkubwa wa gharama na ufuatiliaji wa kinachotokea kila siku.

Makene Ngoroma (33), mkazi wa Kitongoji jirani cha Chikwalaza, anayewajibika na uondoaji taka zinazotupwa hifadhini, ana ushuhuda anaouwasilisha kwa simulizi iliyojaa masikitiko, akitamka:

"Ni kawaida hapa kukuta mizoga ya wanyama barabarani wamegongwa na magari... Mimi niko hapa tangu mwaka 2011 nikitokea Moshi, ni mara chache kupita siku pasiwapo mzoga wa mnyama barabarani.

"Inasikitisha kwa kweli, nyani, swala, nyati wanagongwa na mara moja moja twiga na tembo wanagongwa, nyoka pia wanagongwa sana. Wakati mwingine mnyama anagongwa anasagika kama chapati, inakuwa vigumu hata kumtambua."



Moja ya ajali za barabarani zilizotokea kwenye Hifadhi ya Taifa Mikumi mwaka jana. **PICHA: MAKTABA**

Ngoroma, ambaye pia ni mwanzilishi wa vikundi vya kuokota taka kwenye hifadhi hiyo, anaendelea kufafanua madhara ya ajali hizo akisema:

"Siyo tu kwamba hupunguza idadi ya wanyama wetu hapa kupitia mauaji ya ajali za barabarani, bali pia huharibu mazingira kwa maana ya miundombinu yenyewe ya barabara na usalama wa eneo hili la hifadhi.

"Gari likishagonga mnyama mfano twiga au tembo, mara nyingi linaanguka au kuvunja baadhi ya vifaa vyake hasa kioo kikubwa cha mbele. Hapo sasa kunakuwa na uchafuzi wa mazingira."

Ili kupata ufafanuzi na mapana ya yanayojiri katika kipande hicho cha Barabara ya Tanzania-Zambia, Nipashe iliamua kumdadisi ofisini kwake Mkuu wa MINAPA, Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi Mathew Mombo, anayeweka sawa kwa mtazamo ufuatao:

"Wanyama kugongwa ni moja ya adha kubwa tunazopata hapa kwenye barabara kuu inayopita ndani ya hifadhi. Ni kweli na ni wazi kabisa kwamba magari yanayopita yanasababisha wanyama wetu kugongwa mara kwa mara.

"Ukweli ni kwamba kama kila dereva angekuwa anatembea kwa mwendo elekezi kwenye eneo hili la barabara, wanyama wasingekuwa wanagongwa. Mpaka unamgonga mnyama, ujue kabisa wewe ulikuwa kwenye spidi ambayo siyo sahihi kwako kupita katika eneo hili, lazima utakuwa zaidi ya 50 au 70 (Km 50 au 70 kwa saa).

"Kwa hiyo, tumekumbana na hilo, wanyama wamekuwa wakigongwa, wakubwa na wadogo na mara kadhaa tumewakamata hao watu kwa sababu akimgonga, sheria zinamtaka asimame, abaki hapohapo.

"Wanapokimbia ajali zikitokea, wanasababisha uharibifu wa mazingira lakini pia wanaua wanyama wadogo watambaao.

"Wanaokamatwa wanapigwa faini ya Sh. 50,000 kwa kuzidisha mwendo na wanaogonga wanyama wanalipishwa faini kulingana na thamani ya mnyama ambaye amegongwa.

"Magari yanayopita hapa ni mengi sana kwa sababu magari yote yanayotoka bandarini kwenda mikoa ya kusini mwa Tanzania na nchi jirani za kusini, lazima yapite hapa. Mabasi yanayopita hapa pia ni mengi mno.

"Wanyama wanaoongoza kwa kugongwa ni wanyama wadogo kama swala na nyani kwa sababu idadi yao pia ni kubwa kulinganishwa na wanyama wakubwa kama tembo, twiga au nyati ambao ni mara chache kugongwa japo mwaka huu tayari kuna twiga amegongwa.

"Mara nyingi na kwa kipindi chote tangu nimekuja hapa, madereva wanaogonga wanyama wakubwa kama twiga, huwa wanakimbia na kutelekeza gari baada ya ajali kutokea. Faini zao zimekuwa zikilipwa na wamiliki wa magari husika."

**AONAVYO CAG**

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), pia ana kilio cha kitaaluma namna sekta hiyo inavyohujumiwa.

CAG Charles Kichere, anayewatambulisha wanyamapori kuwa kivutio kikuu cha watalii, anasikitika kwa kutumia takwimu za kitaifa, kwamba sita kati yao, wanauawa kutokana na ajali za barabarani kila siku.

MINAPA ni kati ya hifadhi za taifa 22, ambayo Mhifadhi Mkuu wake, Mombo, anaitambulisha kwamba inashika nafasi ya tisa kwa ukubwa nchini.

Katika ripoti yake ya Ukaguzi wa Mashirika ya Umma Mwaka 2018/19 iliyowasilishwa bungeni Aprili mwaka huu, CAG Kichere anabainisha kwamba wanyamapori 2,266 waliuawa kwa ajali za barabarani ndani ya mwaka huo wa bajeti.

Ni takwimu zinazobeba ujumbe wa kutoweka wanyamapori 189 kila mwezi, sawa na sita kila siku, jambo ambalo CAG analitafsiri kuwa mwelekeo unaopunguza idadi ya wanyamapori, ambao kimsingi ndiyo mtaji mkuu wa utalii.

CAG anafafanua kwamba tatizo hilo linachagizwa na mamlaka husika kuwa na teknolojia duni katika ufuatiliaji wanyamapori, akigusia kukosekana kamera za barabarani, hivyo kushindwa kutambua wahusika wanaosababisha ajali hizo.

"Mapitio yangu ya Ripoti ya Kitengo cha Ulinzi wa Wanyamapori, yaligundua kuwa katika Hifadhi ya Taifa Mikumi (MINAPA), jumla ya wanyamapori 124 wa aina tofauti, waliuawa katika kipindi cha robo tatu ya mwaka (Julai Mosi, 2018 hadi Machi 31, 2019).

"Kutokana na idadi hiyo ya vifo vya wanyamapori mbalimbali, MINAPA ilitakiwa kupokea kiasi cha fedha Sh. milioni 56.64 za tozo na adhabu za kusababisha ajali. Hata hivyo, hifadhi hiyo ilipokea Sh. milioni 12.45 tu, sawa na tofauti ya Sh. milioni 44.18.

"Menejimenti ilieleza kwamba ajali nyingi za barabarani zinatokea wakati wa usiku, hivyo kushindwa kuwaona wanaofanya makosa kutokana na kukosekana kwa kamera za ulinzi.

"Vilevile, katika hali nyingine, malipo yalikuwa yanajadiliwa kutokana na ukweli kwamba Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) halina sheria ndogo za kutoza faini na adhabu, ambapo tozo au faini hutolewa kulingana na Kanuni za Taifa za Uhifadhi wa Wanyamapori, ambazo hazimfungi mtu katika mahakama za sheria," anasema.

Nini kifanyike? CAG ana maoni katika ripoti yake kwamba: "TANAPA na Mamlaka ya Uhifadhi Ngorongoro zitunge sheria ndogo na kuzisimamia ipasavyo.

"Pia, zibuni na kusimamia njia mbalimbali za usalama kama vile kuweka kamera za barabarani, ili kudhibiti ajali za barabarani na hivyo kulinda wanyamapori."

Nipashe ilipoirejea kwa Mkuu wa Mikumi, Kamishna Mombo, kuhusu hoja kutoka Ripoti ya CAG, alisema bado hazijatekelezwa kwa sababu ununuzi wa kamera ni wa gharama kubwa, wakipendekeza hatua hiyo ichukuliwe na wizara mama.

Vivyo hivyo, alifafanua kwamba mara nyingi wameshindwa kuwanasa madereva wa magari wanaosababisha vifo vya wanyamapori kwa sababu wengi hutoroka baada ya tukio.

Hata hivyo, kuna upande wa pili Kamishna Mombo anakiri kupungua matukio ya ajali kwa sasa, ikiwa ni matokeo chanya ya mkakati wa pamoja na mamlaka nyingine za kiusalama, likiwamo Jeshi la Polisi.

Kamishna Mombo, anayeitaja elimu ya umuhimu wa wanyamapori ndiyo suluhisho la kudumu, anasisitiza mtazamo wao mkuu ni usalama wa viumbe vyao, kuliko mapato yatokanayo na faini za ajali hifadhini, zinazofikia kiwango cha juu Dola za Marekani 15,000 (Sh. milioni 34.456) kwa mnyama kama twiga.

Kwa ujumla, bajeti na taarifa za kiserikali zinafafanua kwamba utalii unachangia robo ya pato la fedha za kigeni, huku pia ni md-

INAENDELEA UK. 5

# Barabara zinavyomaliza hazina ya wanyamapori



INATOKA UK. 4

Taifa, ukitoa pia ajira za moja kwa moja 600,000 na zingine milioni mbili zisizo za moja kwa moja.

HATUA ZINAZOCHUKULIWA

Kamishna Mombo anasema katika barabara hiyo inayotumiwa na wanaokwenda katika baadhi ya wilaya za Mkoa wa Morogoro, pia takribani mikoa saba iliyoko Nyanda za Juu Kusini, husababisha kila siku magari kati ya 2,500 na 3,000 kupita ndani ya Km 50 hifadhini Mikumi.

Ili kukabili adha ya ajali hizo, anasema wameanzisha kampeni maalum wakishirikiana na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, Wilaya za Kilosa na Morogoro, wakiwataka madereva wazingatie sheria za hifadhi.

Anaeleza kuwa kampeni hiyo inafanyika sambamba na uongozi wa hifadhi kuongeza doria za usiku na mchana ili kuzuia ajali ndani ya hifadhi, eneo la kimkakati ambalo watalii wa ndani na kimataifa wanafika kuangalia wanyamapori.

Mkuu huyo wa MINAPA anataja sehemu ya udhaifu wa madereva ni kutozingatia maelekezo kutoka kwenye vibao na alama za tahadhari za wanyama wanaovuka barabarani zinazojitosheleza kwa ufafanuzi wa kisheria na kiusalama.

Huku akianika sura pana ya mpango mkakati wa kukabili ajali zinazoathiri wanyama na ustawi wa hifadhi kwa ujumla, Kamishna Mombo anatoa angalizo kwamba kutozingatia sheria kunabeba maana ya kuruhusu ajali endelevu zinazoangukia kupungua wanyamapori.

### POLISI WANAVYOJIPANGA

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Wilbroad Mutafungwa, anasema wameshaanzisha utaratibu wa kufanya ukaguzi wa kila mara, kufuatilia utii wa sheria na kanuni miongoni mwa madereva hifadhini.

"Jeshi la Polisi huwa tunafanya doria za mara kwa mara tukishirikiana na watu wa TANAPA pale Mikumi, lile eneo lote tunalifanyia doria ili kuhakikisha madereva wanaendesha kwa mwendo ulioelekezwa kwenye vile vibao.

"Pia, tunatoa elimu kwa madereva kwa kushirikiana na watendaji wa Mikumi, tumekuwa na mpango wa pamoja wa kuwakumbusha madereva kuzingatia sheria na taratibu zilizowekwa kwenye hifadhi na kuchukua tahadhari.

"Wapo madereva wanaozingatia sheria na wapo wakaidi hasa nyakati za usiku, wanaendesha kwa spidi kali na kuua wanyama. Imekuwa shida siyo tu kwa wanyama, bali hata kwa watumiaji wenyewe wa barabara hiyo kwa sababu gari likimgonga mnyama kama tembo, dereva na watu wengine kwenye gari wanakuwa hatarini.

"Walioweka utaratibu za kuzuia spidi kali mle ndani wana maana kubwa. Tunawaasa madereva wafuate sana sheria zilizowekwa ndani ya hifadhi.

"Tumeweka vituo maalum vya ukaguzi ndani ya hifadhi inapopita barabara ndani ya kilomita 50, ili kuwabaini madereva wanaokiuka sheria za usalama barbarani na zile za hifadhi. Tukiwabaini tunawafikisha mahakamani ili wachukuliwe hatua kali," Kamanda Mutafungwa anaonya.

### KAULI ZA MADEREVA

Madereva waliohojiwa na Nipashe kutoa neno kwa yanayojiri dhidi yao, wana maoni ambayo kwa ujumla yanashikana mkono na mikakati inayoelekezwa na mamlaka hizo za kiserikali.

Dereva wa basi linalofanya safari zake kati ya Dar es Salaam na Tunduma, Mohamed Hussein, anakubaliana na hatua zilizochukuliwa kiserikali, zikiwamo za elimu hifadhini na ufuatiliaji wa uendeshaji wao.

Mwingine anayeendesha basi kati ya Dar es Salaam na Ifakara, Abbas Shaibu, mbali na kutafsiri kwamba kampeni imekuja kwa wakati mwafaka, anawanyooshea kidole baadhi ya wenzake wanaotumia spidi kali, tofauti na inavyoelekezwa hifadhini, hata kuchangia ajali.

Rai yake ni kwamba zitungwe sheria ndani ya hifadhi zitakazowadhibiti anaowaita 'madereva wakorofi', akiamini hatua hiyo ina nafasi ya kupunguza ajali nyingi katika eneo hilo linalolalamikiwa.

### WASIMAMIZI SERIKALINI

Katibu Tawala wa Mkoa wa Morogoro, Dk. John Ndunguru, anataja mkakati wa mkoa ni kudhibiti ajali za wanyamapori na vikwazo vinavyochangia utalii kukwama.

Anasema mkakati huo unahusisha kuweka matatu katika kipande cha Km 50 cha barabara inayopita kwenye hifadhi hiyo ili kudhibiti mwendo wa magari na kutoa elimu kwa madereva na wananchi kuhusu umuhimu wa kulinda wanyamapori walioko hifadhini Mikumi.

"Upo mkakati mwingine mkubwa zaidi ambao uko ngazi ya kitaifa ambao ni kutengeneza barabara inayopita Mikumi kwenda Kilosa mpaka Dumila ambayo moja kwa moja itapunguza ajali ndani ya hifadhi kwa sababu magari hayatapita tena hifadhini.

"Kikubwa, kila mmoja wetu anapaswa kuthamini manufaa ya Mbuga ya Mikumi siyo tu kwa wananchi wa Morogoro, bali pia Watanzania na dunia kwa ujumla.

"Viumbe waliopo eneo hilo ni adimu, kwa dunia ya leo wamebaki katika maeneo machache ambayo unawakuta katika maeneo yao ya asili," anasema.

Kuhusu hatua zinazochukuliwa kukabili kilio hicho kupitia ngazi ya serikali kuu, aliyekuwa Waziri wa Maliasili na Utalii kwenye Baraza la Mawaziri lililopita, Dk. Hamis Kigwangalla, katika ziara yake Hifadhi ya Mikumi, alishaweka wazi tafakuri ya serikali kuona uwezekano wa kubadilisha mwelekeo wa kilomita 50 za barabara, ziwe nje ya hifadhi.

Dk. Kigwangalla alikiri barabara hiyo ya lami haiko katika mazingira rafiki na mbadala mmojawapo uliopo, ni kutoza kodi ya utalii kwa wapitaji.Alifafanua: "Ni barabara ambayo iko 'bize' sana, ni barabara ya kitaifa na kwa vyovyote vile, hii siyo barabara mahususi kwa ajili ya shughuli za utalii.

"Sisi (serikali) tunatafakari namna ya aidha kuiondoa hiyo barabara au namna ya 'kuwachaji' watu wanaokatiza hizi kilomita 50 ambazo zipo ndani ya Hifadhi ya Mikumi."

Dk. Kigwangalla aliwasilisha takwimu kwamba mwaka 2014 wanyamapori waliogongwa walikuwa 351; mwaka 2015 (361); na mwaka 2016 walikuwa 218.

Akizungumza na Nipashe jana, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi wa TANAPA (Idara ya Mawasiliano), Paschal Shelutete, alitaja mambo makuu matatu yanayoandaliwa hivi sasa kukomesha tatizo hilo la ajali za barabarani.

Mosi; Kamishna Shelutete alisema mpango uliopo ni kujenga mageti ambayo magari yatasimamishwa kisha madereva na abiria kupewa elimu kuhusu ulinzi na usalama wa hifadhi.

Pili; alielezea mpango wa kamera maalum kwamba sasa uko katika hatua nzuri kwa ajili ya kufungwa kudhibiti uharibifu huo.

Na mwisho; Kamishna Shulutete alisema mpango wa doria uliopo utaimarishwa kwa kiwango bora zaidi ambacho hakitoi nafasi kwa uhalifu huo wa kusababisha ajali zinazozuilika.

Kuhusu hoja ya CAG kwamba TANAPA iwe na sheria ndogo za kuimarisha ukusanyaji wa mapato yatokanayo na wanyamapori kugongwa barabarani, Shelutete anaanika msimamo wao, akisema:

"Adhabu na kiwango cha faini kinachotozwa tunaamini ni kikubwa. Lengo letu siyo kukusanya mapato, bali kupunguza na ikiwezekana kumaliza kabisa ajali za aina hii."

### MZIZI WA MIKUMI

MINAPA iliyo chini ya TANAPA, iko wilayani Kilosa mkoani Morogoro, umbali wa kilomita 283 magharibi mwa Jiji la Dar es Salaam na kilomita 311.7 kaskazini mwa Mbuga ya Selous (Hifadhi ya Taifa ya Nyerere), ambayo ni kubwa kuliko zote nchini.

Kwa mujibu wa Kamishna Mombo, Mikumi ni kitega uchumi kilichoanzishwa kisheria mwaka 1964, kikiwa na ukubwa wa kilomita za mraba 1,070 na baadaye mwaka 1975, serikali iliongeza maeneo yake ya kusini na kaskazini hata kuwa na kilomita za mraba 3,230.

### USULI & HISTORIA

Sera ya Wanyamapori ya Tanzania (2007) inabainisha kuwa historia ya uhifadhi wa wanyamapori nchini ilianzia mwaka 1891. Kwa lugha rahisi, ni miaka 129 iliyopita au karne moja na robo.

Hiyo ilikuja kama matokeo ya kuzaliwa kwa sheria za kudhibiti uwindaji zilizoanzishwa na utawala wa Kijerumani uliokuwapo katika zama hizo.

Kwa kurejea sera iliyopo sasa, sheria hizo za awali zililenga kudhibiti uvunaji holela wa wanyamapori; kuhakiki mbinu za uwindaji na biashara ya wanyamapori waliokuwa hatarini kutoweka.

Hifadhi ya kwanza ya wanyamapori nchini ilianzishwa na Wajerumani hao miaka 14 baada ya kutunga sheria katika ukanda wa hifadhi maarufu ya sasa iitwayo Pori la Akiba Selous, mwaka 1905.

Sera inafafanua kwamba kanuni za kitaalamu zilizotumika kuteua maeneo ya hifadhi za wanyamapori, zilizingatia vigezo kama kuwapo wanyama wakubwa pekee na siyo mengine ya ziada yanayotawala sasa, kama makundi yao ya baionuai za kibaiolojia.

Baada ya kupita miaka 16 ya hifadhi kuanzishwa, Tanganyika ikiwa chini ya utawala wa mkoloni mpya, Uingereza, mwaka 1921, kukaanzisha Idara ya Wanyamapori sambamba na mwaka mmoja baadaye, serikali ililitangaza rasmi Pori la Akiba Selous.

Idara hiyo ya wanyamapori ilikasimiwa majukumu ya kiutawala kuhusu usimamizi wa mapori ya akiba, kutekeleza kanuni za uwindaji na kuhakikisha watu na mazao yao hawaingiliwi au kuvamiwa na wanyama.

Sera inafafanua kuwapo historia ya ushuhuda wa hifadhi nyingine mbili kuanzishwa miaka sita baada ya hatua ya mwisho mwaka 1922.

Hapo panatajwa iliyokuwa Bonde Kuu Funge la Ngorongoro (sasa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro) na Pori la Akiba Serengeti (sasa Hifadhi ya Taifa Serengeti).

| Mnyama | Dola | Sh. milioni |
|---|---|---|
| Tembo | 15,000 | 34. 716 |
| Nyati | 1,900 | 4.397 |
| Simba | 4,900 | 11.341 |
| Chui | 3,500 | 8.1 |
| Twiga | 15,000 | 34.716 |
| Fisi | 550 | 1.273 |
| Ngiri | 450 | 1.041 |
| Nyani | 110 | 0.255 |
| Pundamilia | 1,200 | 2.777 |
| Swala | 390 | 0.903 |

Faini wanazotozwa madereva wanapogonga wanyamapori Hifadhi ya Taifa Mikumi (MINAPA). **CHANZO: MINAPA, NOVEMBA 6, 2020**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Huduma za upimaji, tiba ya saratani zifike wilayani

**KATIKA** kuelekea maadhimisho ya Siku ya Mionzi Duniani ambayo hufanyika Novemba 8, kila mwaka, kumekuwa na shughuli mbalimbali zikiwamo elimu ya afya hususan magonjwa ya saratani pamoja na upimaji.

Shughuli hizo ambazo hufanyika bila malipo kwa ushirikiano kati ya serikali na taasisi mbalimbali zikiwamo binafsi, watu hujitokeza kupima afya huku baadhi wakigundulika kuwa na maradhi ya saratani.

Awali, maadhimisho hayo yalikuwa yakifanyika kwenye maeneo mbalimbali kwa wataalamu kufanya huduma. Hiyo ilikuwa ni kutokana na Taasisi ya saratani ya Ocean Road (ORCI) ya jijini Dar es Salaam kutoa huduma hizo lakini katika kuhakikisha wigo wa huduma unakuwa mpana, Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Bugando ya jijini Mwanza, nayo imeanza kufanya upimaji na tiba.

Katika maadhimisho ya mwaka huu, zaidi ya wananchi 300 katika mikoa mbalimbali ya Kanda ya Ziwa, wamejitokeza katika huduma hiyo ya upimaji afya bure Bugando kwa siku mbili mfululizo. Miongoni mwa vipimo walivyofanyiwa ni homa ya ini, saratani, tezi dume kwa wanaume na kansa ya shingo ya kizazi kwa wanawake.

Kutokana na wingi wa watu kufuata huduma za upimaji, Daktari Bingwa wa Mionzi katika Hospitali hiyo, Magreth Magambo, akizungumza wakati wa upimaji huo, alisema kuna haja huduma hiyo kusogezwa hadi ngazi ya wilaya ili kutoa fursa kwa wananchi wengi.

Dk. Magambo alisema katika upimaji huo pekee watu kadhaa wamegundulika kuwa na tezi dume, kansa ya kizazi na homa ya ini. Hali hiyo inaonyesha kuna umuhimu mkubwa serikali kwa kushirikiana na wadau wa afya, kuongeza kasi ya upatikanaji wa huduma katika maeneo mbalimbali nchini.

Kwa sasa, mathalan, huduma za upimaji wa magonjwa ya saratani zinapatikana Mwanza na jijini Dar es Salaam jambo ambalo ni vigumu kwa wananchi wengi, ambao uwezo wao kifedha ni mdogo, kuzipata.

Hata hivyo, serikali haina budi kupongezwa kwa kupeleka huduma hizo Mwanza na ni imani kuwa zitapunguza kwa kiasi kikubwa gharama za watu wanaohitaji vipimo na tiba kwa sababu awali walikuwa wakizifuata Dar es Salaam.


Kama ilivyobainishwa na wataalamu wa afya kwamba asilimia 40 ya wagonjwa wa kansa wanatoka mikoa ya Kanda ya Ziwa, kutokana na kuwa na hazina kubwa ya madini ambayo yanachangia kwa kiasi kikubwa ongezeko la maradhi hayo, kuna umuhimu mkubwa kwa huduma hiyo kupanuliwa huku nguvu kubwa ikaelekezwa katika mikoa hiyo.

Ikumbukwe kwamba Kanda ya Ziwa ina mikoa mingi kulinganisha na maeneo mengine ya nchi, hivyo huduma za upimaji afya na tiba ya maradhi ya saratani ikipewa kipaumbele katika eneo hilo, ni imani kwamba maisha ya wengi yatasalimika.

Tunasema hivyo kwa sababu elimu itatolewa kwa kiwango kikubwa na watu watajitokeza na hatimaye kupimwa na wale watakaobainika kuwa na maradhi hayo, watapatiwa huduma haraka na hatua hiyo itapunguza ongezeko la magonjwa na hata vifo.

Katika kuhakikisha jitihada za kupunguza maradhi na hata vifo vitokanavyo na saratani, kwa kuanza, serikali inaweza kuanza na hospitali za rufani za kanda kama vile KCMC (Moshi), Mbeya, Benjamin Mkapa (Dodoma) na Mtwara na baadaye hospitali za rufani za mikoa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Sekondari zimejipangaje kupokea kidato cha kwanza mwaka 2021?

**MWAKA** wa tano sasa unaelekea ukingoni tangu wanafunzi wa shule za msingi na sekondari waanze kufaidi matunda ya elimu bure baada serikali kuamua kubeba mzigo wa gharama na kuwapa nafuu wazazi na walezi.

Hatua ya serikali kugharimia elimu, imekuwa fursa kwa wazazi na walezi waliokuwa wamekata tamaa ya kusomesha watoto wao kwa kushindwa kulipia ada, kuwaandikisha na kuanza masomo.

Kwa mara ya kwanza, ilielezwa kuwa idadi ya watoto walioandikishwa Desemba, 2015 kwa ajili ya kuanza darasa la kwanza mwaka 2016, ilikuwa kubwa kuliko miaka ya nyuma.

Inaaminika kwamba kwenye mafanikio, matatizo nayo huwa hayakosekani, hivyo pamoja kuandikishwa kwa watoto wengi, limekuja tatizo la uhaba wa vyumba vya madarasa katika shule mbalimbali zikiwamo za msingi na sekondari.

Tatizo hilo huwa linaibuka kila mwaka na kusababisha baadhi ya wanafunzi kusomea chini ya miti au kwenda shuleni kwa zamu ili kuepusha mlundikano madarasani.

Njia nyingine inayotumika ni wanafunzi kuanza masomo kwa mafungu, wakiwamo wale wanaosubiri hadi madarasa yamalizike kujengwa huku baadhi wakiwa tayari wako shuleni.

Kwa mazingira kama hayo, ni wazi kwamba baadhi yao watakuwa nyuma kimasomo wakati wengine wameshapiga hatua, hivyo umefika wakati sasa wa kuvalia njuga ujenzi wa madarasa ya kutosha katika kila shule.

Mfano, wanafunzi 100 wanaweza kuchaguliwa kujiunga na sekondari fulani, lakini kutokana na uhaba wa madarasa, watachukuliwa baadhi na kuanza masomo, huku wengine wakisubiri madarasa mengine zaidi yajengwe.

Hapa ni wazi kwamba wale waliofanikiwa kuanza masomo mapema watawaacha mbali wenzao, hali inayoweza kusababisha wasiwe na uelewa wa masomo unaolingana, ingawa wako kidato kimoja.

Mwaka huu, wanafunzi 1, 024, 007 walifanya mtihani wa taifa wa darasa la saba na baadhi yao wanatarajia kufaulu na kuendelea na masomo ya sekondari, hivyo suala la ujenzi wa vyumba vya madarasa halikwepeki.

Inawezekana wako wanafunzi ambao wazazi wao watawapeleka katika shule binafsi, lakini wengi ni wale watakaosoma katika sekondari za umma ambazo nyingi zinakabiliwa na uhaba wa madarasa.

Kwa kuwa ni shule za umma na kwa kuwa umma ndiyo jamii yenyewe, haina budi kuhakikisha zinakuwa na madarasa ya kutosha ili kuwaepusha wanafunzi na matatizo ya kila mwaka ambayo yako ndani ya uwezo wa jamii.

Binafsi ninaamini kwamba wazazi wakiamua kugawana majukumu ikiwamo kutoa nguvu kazi zao, wanaweza kusaidiana na serikali kujenga madarasa ya kutosha katika shule mbalimbali za sekondari nchini.

Kwa mfano, shule ya sekondari ya kata inaweza kuwa inahudumiwa vijiji hata vinne, hivyo si vibaya wazazi wa vijiji hivyo wakakubaliana kila kimoja kujenga darasa moja na kujikuta wamekamilisha manne.

Mtindo wa aina hiyo uwe endelevu, kwa ajili ya kuwa na madarasa mengi badala ya kusubiri matokeo ya madarasa ndipo hatua zichukuliwe. Kwa kuwa kufanya hivyo itakuwa kuendelea kukumbatia tatizo.

Utoaji wa elimu bure na pia wingi wa shule za sekondari za kata, kwa kiasi kikubwa umesaidia familia zisizo na uwezo kiuchumi kufaidika kwa kuwa zamani zilikata tamaa kutokana na kukosa fedha za kusomesha watoto.

Lakini juhudi hizo za serikali zinakwamishwa na uhaba wa madarasa, hivyo kwa kuwa shule ni za umma, basi umma nao ufanye sehemu yake katika kufanikisha ujenzi wa madarasa.

Kwenye baadhi ya maeneo nchini, wapo baadhi ya wazazi na walezi, ambao hawataki kusikia mambo ya kujitolea kujenga madarasa, hata kuchangia maendeleo ya shule, kwa kuwa wanaamini serikali ilishafuta michango.

Mawazo kama hayo, hayatakiwi kupewa nafasi, hasa kwa kutambua kuwa shule hizo ni mali ya umma, hivyo wao kama umma, wana wajibu wa kuzihudumia, si kusubiri serikali ifanye kila kitu.

Kwa kuendekeza mawazo hayo, imefikia hatua hata choo cha shule kikibomoka, baadhi ya wazazi na walezi wanasubiri serikali ijenge wakisingizia kuwa ilishatangaza kutoa elimu bure, hivyo wao hawahusiki katika hilo.

Watu wenye mtazamo huo wanachangia kukwamisha maendeleo ya shule, hawana budi kubadilika na kutambua kuwa wana mchango mkubwa katika maendeleo ya shule, hivyo wasijiweke pembeni.

SAFU

## FIKRA MBADALA



Nkwazi Mhango, Canada

# Matokeo ya uchaguzi wachache tuliona kilichowashinda wengi

NILIPOANDIKA makala "Kwa mtaji huu upinzani utashindwa tu" muda mfupi kabla ya kupiga kura kuwa wapinzani wangeshindwa vibaya, wapo walioniona kama mtu anayejipendekeza kwa chama tawala wasijue ukweli utasimama tena si baada ya kitambo kirefu. Sasa matokeo yametoka, na ukweli umejulikana.

Uyakubali hata uyakatae, waliodhani nilikuwa nakipendelea chama tawala hawana la kusema bali kushangaa ilikuwaje japo ilikuwa rahisi kutabiri kipigo kilichotokea. Hata kama hupendi kitu, kusema ukweli ni sehemu mojawapo ya kukusaidia kufikisha kile unachoamini au kutaka kuwasilisha. Pia kuukubali ukweli husaidia kimkakati kupambana na kile unachotaka kupambana nacho kisayansi na si kwa kujilisha pepo au kutegemea miujiza.

Kwa wanaojua namna Watanzania walio maskini wanavyomuunga mkono Rais John Pombe Magufuli, hawakushangaa kwangu kutabiri kuwa chama tawala kingeshinda ki-Tsunami. Hii ni kutokana na sababu zifuatazo:

Mosi, wengi wa wapiga kura ni wakazi wa vijijini wakilinganishwa na wasomi wachache wa mijini ambao mara nyingi ndiyo wanaounga mkono upinzani ukiachia mbali kuwa uzoefu unaonyesha kuwa wengi hawapigi kura. Mfano, mzazi ambaye mtoto wake sasa anasoma bure huwezi kumshawishi akuchague na kumuacha aliyewezesha mwanawe kupata huduma hii. Raia ambaye tangu taifa lipate uhuru zaidi ya miaka 60 iliyopita bila kuona barabara ya lami au bomba la maji, huwezi kumshawishi akuchague amuache aliyewezesha kupatikana kwa huduma hizi tena ndani ya miaka mitano tu?

Pili, mwanakijiji ambaye tangu tupate uhuru ameishi kwa kibatari halafu ghafla, ndani ya miaka mitano, akapata umeme huwezi kumwambia kitu.

Kama kuna siri ya wapinzani kuangusha vibaya, si nyingine bali hii. Wapo waliokejeli kuwa Watanzania sasa wanasifia, barabara, flyover, kusambazwa umeme, mabwawa ya kuzalisha umeme, madaraja, meli, ndege, reli, umeme na mengine mengi. Je, walitaka wasifie nini wakati hizi ni nyenzo za maendeleo?

Tatu, mama aliyekuwa akijifungulia nyumbani au kwenye zahanati inayotegemea kibatari asingeweza kuchagua yeyote zaidi ya yule aliyewezesha kupatikana huduma ya uhakika. Mamantilie aliyekuwa akimwagiwa chakula chake na migambo au machinga akifukuzwa na kukamatwa ovyo ovyo asingemchagua yeyote zaidi ya aliyekomesha kadhia hizi.

Mwananchi mchukia rushwa asingeweza kumchagua mwingine zaidi ya yule aliyeikomesha. Aliyekuwa akisafiri kupitia nchi jirani kwenda Dar asingemchagua yeyote zaidi ya aliyetatua tatizo lake.

Nne, mwananchi aliyekuwa amekosa kazi tokana na ajira nyingi kuchukuliwa na walioghushi au kutolewa kikabila, asingeacha kuchagua aliyekomesha kadhia hizi.

Hapa hatujaongelea usalama kwa ujumla. Mikoa iliyozoea kutekwa kwa magari usiku na kushamiri kwa vitendo vya ujambazi asingechagua wapinzani hata wangemwimbia mashairi mazuri kiasi gani.

Tano, ukizingatia ukweli hapo juu, utagundua kuwa hata malalamiko juu ya matokeo ya uchaguzi uliokwisha na kukipa chama tawala ushindi mnono, yatahitaji ushahidi wa nguvu kweli kweli kusimamisha kesi ya msingi.

Kwani, madai yanayotolewa kwa sasa, kimahesabu ya kura na matokeo, yanakosa uzito japo hatupingi kulikuwa na matukio yaliyoripotiwa bila kutolewa ushahidi.

Hii ni kazi ya mahakama; si kazi ya uchambuzi. Tunaambiwa kura za urais za Magufuli ameshinda kwa kura zaidi ya 12,000,000 dhidi ya mpinzani wake wa karibu aliyepata kura takriban 1,000,000.

Hii maana yake nini? Je, mshindi alipewa kura ngapi feki au tuseme mshindwa aliibiwa kura ngapi? Wangepishana kura kama elfu kadhaa, madai ya wizi wa kura yangeweza kujenga ushawishi hata kama yangekuwa ya kuzua. Kwa hali ilivyo, tukubali, upinzani umeshindwa vibaya ikilinganishwa na uchaguzi wa kabla.

Tulishaeleza ni kwanini upinzani ulifanya vizuri katika uchaguzi wa mwaka 2015 ambazo tunaweza kufupisha kuwa ni kama ifuatavyo:

Mosi, chama tawala kilikuwa kinamekumbwa na kashfa kibao ukiachia mbali kutamalaki kwa rushwa wakati ule ikilinganishwa na sasa ambapo serikali iliyochukua madaraka baada ya hapo ilifanya mageuzi makubwa kisiasa na kiuchumi hata ndani na nje ya chama tawala na serikali yake.

Pili, katika uchaguzi wa mwaka 2015, mgombea wa chama tawala aliyeshinda alikuwa ndiyo mara yake ya kwanza kupitishwa kugombea nafasi hiyo tena akishindana na mgombea wa upinzani aliyekuwa na uzoefu na jina kubwa kuliko yeye.

Tatu, Watanzania walikuwa wamezoea siasa za mazoea. Baada ya kuonja mafanikio ya muda mfupi kama vile kuingia kwenye uchumi wa kati, kurejesha tunu zilizokuwa zimepotea muda mrefu kama Shirika la Ndege la Taifa la Air Tanzania, kufumua mfumo uliokuwa umeoza kwa ufisadi, ukabila, mazoea na wizi, huwezi kuwaambia kitu wala kuwarudisha nyuma.

Nne, kimsingi Watanzania hawakuwa na mahitaji au maswali mengi kwa serikali au anayetaka kuwaongoza ikizingatiwa ukweli kuwa serikali iliyokuwa imemaliza muda wake ilikuwa imejibu karibu maswali yote na ya ziada kiasi cha kuwafanya waridhike nayo; na hivyo kuiamini miaka mitano mingine.

Mwisho, chama tawala kiliendesha kampeni za kisayansi kikiahidi 'maajabu' zaidi ya yale ambayo Watanzania wengi walikuwa wamekishangaa na kuridhika nayo.

Kimsingi, badala ya wapinzani kulalamika, wajipange upya kutegemeana na mambo yatakavyo kuwa kwenye miaka mitano ijayo. Ni ushauri wa bure.

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Hakika CCM kama nyani mzee!



Na Joseph Kulangwa

SIKU hizi vijana au watoto hawana fursa ya kusomewa vitabu vya hadithi au hata kusimuliwa hadithi na wazee wao. Kusimuliwa na mababu na mabibi zao, wakiwa wanaota moto usiku wakisubiri chajio.

Badala yake wanakalia zaidi kusikiliza muziki wa kizazi kipya, wanakalia bongomuvi, wanashindana mavazi na kurushana kwenye mitandao ya kijamii, bila kujua kuwapo kwa historia ya jamii zao.

Wangezingatia simulizi mbalimbali wanazopewa na hata kusoma vitabu kama vya Adili na Nduguze, Mashimo ya Mfalme Suleiman, Kisiwa cha Giningi, Rosa Mistika, Pepo ya Mabwege, na vingine vya aina hiyo, wangeshajifunza mengi wala wasingepata tabu, hasa katika nidhamu.

Wangesoma Mashimo ya Mfalme Suleiman, wangekumbana na usemi wa kujitambulisha wa Umsolopagaaz, wa kabila la Wazulu na damu ya Chaka, Mkuu wa Majeshi ya Nkomabakos, akiapa kutumia pigo moja lililonyooka la shoka na kumaliza mambo.

Kwa Umsolopagaaz kazi ilikuwa ni moja tu, ya kupiga na kusambaratisha maadui. Hicho ndicho nilichokiona katika uchaguzi wa urais, ubunge na udiwani na hata uwakilishi mwaka huu katika Tanzania.

Pigo moja lililonyooka la shoka, hakika limesambaratisha upinzani nchini. Mpaka sasa ngumu kuamini kilichotokea, kwamba CCM imeweza kusambaratisha wapinzani kiasi hiki cha kutishia Bunge kureja kuwa la chama kimoja!

Ukiuliza walioko upande wa washindi, watakwambia kirahisi sana, kwamba ni sera nzuri na yaliyofanywa na awamu hii ya tano katika muhula wake wa kwanza. Lakini wale wa upande wa pili nao haraka tu, watakwambia wameibiwa. Mimi ambaye niko katikati, nitasema tu kwamba uchaguzi umemalizika, aliyeshinda kashinda na aliyeshindwa kashindwa. Nitakwambia tu kwamba kila ushindani na mbinu na ujanja wake, ukizubaa umeliwa.

Hata kwenye soka, tunajua, mbona Wabongo tunapenda sana soka, na ndiyo sababu tumegawanyika katika usimba na uyanga, na tunajua kuna magoli ya mkono. Ukizubaa limo.

Sijajua kama wapinzani walizubaa likawamo, au kama washindi ambao ni watawala kweli walilitumbukiza kwa mkono bila msimamizi, yaani mwamuzi, Waitu Kaijage na wenzake, wakashindwa kuona au wakaona wakauma filimbi!

Kwenye soka, tunajua ngoma ikimalizika wachezaji hukumbatiana na kuyaacha hapo, hata Malkia Sendiga alisema kwenye ngumi nako ni hivyo hivyo, mnatwangana mnatoana ngeu, lakini mwisho wa siku mnakumbatiana na maisha yanaendelea.

Kina Tundu wanaona ukakasi kabisa kukumbatiana na kina Pombe, pengine wanadhani wenzao waliweka mawe kwenye glovu, au walifunga magoli kwa mkono. Sasa sijui kamati ya saa 72 inaweza kufanya nini katika hilo!

Tatizo watu wanasahau kuwa hili lisisiemu ni nyani zee lililokwepa mishale, mikuki, magobori, mapanga na hata mawe lukuki, hivyo linajua mbinu zote za ushindi, sasa ukiingia kichwakichwa hujui mishale ya sumu na isiyo na sumu ni ipi, itakuua tu.

Hebu tazama sasa, Pombe katupa makonde kadhaa 12 yametua usoni mwa Tundu, huku Tundu akirusha ya kwake na ni moja tu lililotua, nani atashinda? Lazima Pombe amleweshe Tundu tu atake asitake.

Sasa watazamaji nao wana yao, wanajiuliza, hivi hii tofauti ya kura milioni 12 na milioni moja, si maajabu haya? Wanakumbuka 2015 ambako angalau tofauti ilikuwa ya milioni nane kwa milioni sita! Tena safari hiyo Edo hakuwa msemaji sana kama alivyokuwa Tundu kwenye kampeni za mwaka huu.

Kama ni nyomi mwaka huu, kila upande ulikuwa na nyomi yake, tena mmoja ukihanikiza wasanii wote uwajuao wa nji hii, huku mwingine ukichechemea, lakini bado nyomi zilikaribiana na kujiaminisha kuwa safari hii chuma kikoli moto.

Lakini wapi bwana, Mzee wa Chato akachukua 12 kati ya 14 na zilizobaki mbili akawaambia haya gawaneni huko, ili mbaki na ushahidi kuwa nanyi mlishiriki na kwamba kuna watu walikupigieni! Aisee, zereu duh! Wabongo tujiulize na tujifunze kwa kilichotokea uchaguzi huu huru na wa haki! Alamsiki!

## KONA YA UKWELI

# Uchaguzi umekwisha sasa tuchape kazi



Na Thobias Mwanakatwe

NOVEMBA 5, 2020 Jiji la Dodoma kwa mara ya kwanza lilishuhudia tukio muhimu la kuapishwa kwa Rais John Magufuli kuendelea kuongoza nchi katika serikali ya awamu ya tano tangu Uhuru.

Hatua ya kuapishwa Dk. Magufuli ilikuwa kuhitimisha kipindi cha kwanza cha uongozi wa awamu ya tano, na kuanzisha kipindi cha pili cha awamu hiyo cha kuwatumikia Watanzania.

Baada ya kiapo hicho, linabaki jambo moja kubwa na muhimu mbele yetu kama taifa, kuchapa kazi kwa bidii ili kuijenga Tanzania mpya ambayo kila mtu anaitamani.

Kama alivyosema Rais Magufuli, uchaguzi umekwisha kwa hakika umekwisha sasa siasa zetu zitafsiriwe kwa kazi, tuanze kuishi falsafa ya siasa ni kazi. Huu si tena wakati wa kupiga siasa za maneno na blabla vijiweni.

Miaka mitano ya Rais Dk. Magufuli madarakani, imedhihirisha wazi kwamba maendeleo ya kweli yanaletwa na kazi. Ukichapa kazi kwa bidii na nidhamu kubwa unajihakikishia ustawi. Tanzania imepiga hatua kubwa katika kipindi cha miaka mitano iliyopita kutokana na falsafa ya kufanya kazi kwa nidhamu na maarifa.

Ili Rais Magufuli atekeleze vyema ahadi za Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), ni lazima wote sasa tushikamane na kuelekeza nguvu na juhudi zetu katika kuunga mkono utekelezaji wa ilani hiyo.

Ukubwa wa ilani ya CCM una maana moja kwamba yako mambo mengi ambayo chama kimeahidi na ambayo pia Watanzania tunatamani yatekelezwa kwa wakati ili ile Tanzania mpya tunaoitamani iweze kuwa halisi kwa maslahi na ustawi wa maendeleo ya watu wetu.

Ukubwa wa ilani hiyo pia una maana moja kubwa sana, baada ya uzoefu wa miaka mitano na kuona jinsi ambavyo katika kipindi hicho CCM kimeweza kutekeleza mambo makubwa mengi kwa mafanikio makubwa.

Ni matumaini ya Watanzania wote kwamba Rais Magufuli, kama ilivyo kawaida yake, ni mtu wa vitendo, analoahidi anatekeleza, kwa hiyo mambo mengi yaliyoahidiwa katika ilani ile yatageuka kuwa halisi ndani ya miaka hii mitano ya kipindi cha pili cha awamu ya tano.

Ni jukumu letu sasa kama wananchi, kwanza wale ambao hatujabadili mitazamo yetu kuhusu utendaji kazi wa Rais Dk. Magufuli, tuanze sasa kubadili fikra zetu, tutambue kwamba huyu ni mtu wa kazi.

Kwa mantiki hiyo, ili maisha yawezekane kwa kila mmoja wetu lazima tuwe na mtazamo huo huo wa kuchapa kazi. Kazi ni kipimo cha utu, tifaye kazi kwa bidii na nidhamu kwa manufaa yetu na taifa letu.

Lakini pili, nidhamu na kuwa wazalendo wa kweli Taifa letu. Kinachomsukuma Rais Magufuli kuchapa kazi kwa bidii na kusimamia kwa nguvu zote rasilimali za taifa letu ni uzalendo.

Watanzania ni lazima tuone fahari kwa mambo yetu, tujivunie Magufuli wetu, tujivunie kazi zake, tuone fahari na matokeo ya kazi hizo, tuyalinde na kuyatunza mafanikio yaliyopatikana wakati tukiendelea kujenga zaidi juu ya mafanikio hayo.

Kiapo cha Mheshimiwa Rais Magufuli kiwe chachu ya kuamsha uzalendo wetu kwa taifa letu, tushikamane kwa dhati katika jitihada za kuendelea kuijenga Tanzania yetu, namna pekee ya kulifikia hili ni kuungana na kushikamana kama taifa, nyuma ya Rais Magufuli katika kutekeleza yale yote aliyoyaahidi.

Nampongeza Rais Magufuli kwa heshima aliyopewa na Watanzania kuwaogoza tena katika kipindi cha miaka mitano ijayo.

Hongera sana Mheshimiwa Rais, umetenda kazi imeonekana, Watanzania wameonyesha shukrani zao kwa kukupa ushindi wa kishindo, wana imani na wewe wana imani na za kazi zako. Sasa jambo letu ni moja tu, kazi iendelee.

**MUNGU IBARIKI TANZANIA, MUNGU MBARIKI RAIS DK. JOHN MAGUFULI**

**Kwa ushauri na maoni tumia barua pepe mwanakatwe2015@gmail.com**

## DARASA LA NDOA

# Kutenga muda wa kazi na familia chachu ya ufanisi -2



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka 0744000066

JUMAPILI iliyopita tulizungumzia kwa kina juu ya umuhimu wa rasilimali watu mahali pa kazi na kwamba mafanikio yoyote mahali pa kazi yanategemea watu. Na ili mafanikio hayo yawe ya kweli, jambo la msingi ni kuwa na wafanyakazi wenye furaha.

Furaha na utendaji kazi kwa ufanisi mahali pa kazi, kimojawapo kinapokosekana basi hakuna tija na ufanisi mahali pa kazi. Kutokana na ukweli huo, waajiri wamekuwa wakiwekeza katika huwajengea uwezo wafanyakazi na watumishi wao na kujitahidi kuhakikisha wana furaha siku zote.

Zaidi ya hayo, ili mfanyakazi afanye kazi kwa amani na furaha na hatimaye kuwapo mafanikio katika kazi yake na taasisi kwa ujumla, ni lazima pia familia yake iwe na furaha.

Kama nilivyoeleza katika makala iliyopita, wafanyakazi wakiwa na matatizo ya kiuhusiano kazini na nyumbani, hali hii kwa sehemu kubwa huathiri kiwango cha furaha na utendaji wao wa kazi.

Kunapotokea matatizo ya ndoa na uhusiano kwa mfanyakazi, msongo wa mawazo ni lazima. Hii humwathiri mfanyakazi kisaikolojia, kiafya, kimwenendo na ufanisi katika utendaji wa kazi na hatimaye kusababisha hasara kwa taasisi.

Kwa mantiki hiyo, ifahamike kwamba ndoa au uhusiano huchangia kwa kiasi kikubwa matokeo ya utendaji kazi na ustawi wa taasisi. Kunapokuwa na matatizo katika ndoa au uhusiano, ni dhahiri ufanisi utakuwa mbovu. Pia kunapokuwa na furaha na amani katika ndoa au uhusiano, tija na ufanisi mahali pa kazi ni lazima vitapatikana.

Kutokana na ukweli huo, mfanyakazi anapokuwa na familia yenye furaha na amani, ni hakika mambo katika sehemu yake ya kazi yatakuwa mazuri. Kwa hiyo, ili mfanyakazi au mtumishi afanye kazi kwa ustadi na weledi, lazima apate muda wa kuwa karibu na familia.

Ndoa, kama tunavyoelewa, ni kiini cha familia, jamii na taifa. Hivyo, ndoa zikiwa imara, tutakuwa na familia, jamii na taifa imara. Ndoa imara huleta tija mahali pa kazi. Kazi na familia hutegemeana.

Hivyo, ili ndoa iwe na amani na furaha na pia kuwe na ufanisi kazini, ni lazima mtu atenge muda wa kazi na ule wa kuwa na familia. Kama nilivyodokeza katika makala iliyopita, kwani nguvu kubwa ikielekezwa katika kazi, kuna uwezekano mkubwa wa kusahau familia.

Vivyo hivyo, nguvu kubwa ikielekezwa katika familia na kusahau majukumu ya kikazi, hili nalo ni tatizo.

Kutokana na hali hiyo, Ili kuwa na muda wa kazi kwa upande mmoja na familia upande mwingine, ni muhimu kuzingatia mambo yafuatayo:

Kwanza, kujali muda na kuacha kuishi kwa mazoea. Siku zote tatizo si muda, bali namna ya kutumia muda tuliopewa. Watu wengi wana tatizo la matumizi ya muda. Hakikisha muda wa kazi unautumia kwa kazi na siyo mambo mengine nje ya kazi. Zingatia muda wa kuingia na kutoka kazini.

Halikadhalika muda wa familia, utumike kwa ajili ya familia. Kwani lipo tatizo kwa baadhi ya wafanyakazi kutumia muda wa kazi kwa mambo mengine yasiyohusiana na kazi, hivyo, kujikuta muda ambao ungetumika kuwa na familia, unatumika kwa kazi za ofisini.

Pili, kujiwekea mipaka na vipaumbele. Si lazima kufanya mambo yote kwa siku moja, kwani hata kesho ipo pia. Jifunze kupangilia kazi zako kwa kuzingatia vipaumbele.

Tatu, kutunza nidhamu ya matumizi ya simu yako ya mkononi. Kuna baadhi ya watu ni watumwa wa simu zao za mkononi. Wakati wote wanashughulika na simu. Simu yako ya mkononi isiibe muda wa mwajiri wako au familia yako.

Ni muhimu kujua ni mahali gani na nyakati zipi za kutumia au kutokutumia simu yako. Pia jifunze au jenga mazoea ya kuitelekeza simu yako wakati mwingine ili usiharibu kazi na uhusiano wako na familia au mpenzi wako.

Nne, hakuna budi kujifunza kusema hapana. Usiwe mtumwa wa matukio au marafiki. Kila mahali unataka kwenda. Ukiambiwa twende huku au kule unakwenda. Hujui kukataa na huna vipaumbele. Kuna mambo ya kusema hapana.

Muda na familia yako niwa thamani sana. Pangilia muda wako kwani mumeo, mkeo, mtoto au watoto wako ni watu muhimu sana na wawe kipaumbele chako. Thamani yako kwao inategemea muda unaowekeza kwao.

Tano, kutengeneza Tengeneza muda wa kuwa na familia. Muda usipotengenezwa hauwezi kuja. Dhamiria kutengeneza muda wa kuwa na familia unapatikana. Tengeneza muda ili usiwe mgeni wa familia na nyumba yako kila siku.

Kazi zisiwe kisingizio cha kudumu cha kukosa muda na mwenzi wako au familia yako. Msingi wa familia ni pale wanandoa wanapopata muda wa pamoja.

Sita, nafasi zetu za kazi zibaki mahali pa kazi na si kwenda nazo mpaka nyumbani. Ukiwa nyumbani tambua kuwa wewe ni mke aumume wa mtu na baba au mama wa familia. Timiza wajibu wako wa nyumbani ili thamani ya uwapo wako iongezeke kwa mkeo au mumeo pamoja na watoto.

■ **Dk. Mlyuka ni Mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishughulisha na masuala ya ndoa na malezi. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa:** info@tamcare.or.tz

# MAISHA

NOVEMBA 8, 2020
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili



Ukurasa 14

**Kula nyanya chungu upate faida kiafya**



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Athari udongo wa mfinyanzi katika ujenzi wa nyumba



## HARUSI

Ukurasa 12



## 'CONCEALER' Kipodozi kinachompa ujana mwanamke

Ukurasa 14

# Kweli dada wa kazi amemuweza mwanao?

**Na Moses Ismail**

BADO ni mtoto mdogo sana, wa miaka mitatu au pengine anakaribia miaka minne. Kwa umri wake, hana uwezo wa kujieleza kwa maneno kwa jambo lolote analolitaka.

Lakini wewe kama mzazi, unazifahamu tabia zake. Ni mbishi wa kula, huwa hali mpaka aimbiwe nyimbo zote unazozijua na wakati mwingine mnazungushana nyumba nzima.

Dada wa kazi aliyeondoka hivi majuzi, ndiye aliyemlea tangua alipozaliwa. Wamekuwa 'wakihangaishana' sana juu ya tabia zake hizo za kukataa kula na wakati mwingine kulilia vitu kadhaa ambayo dada pamoja na wewe humkataza 'asivichezee' kwa kuwa ni vya hatari.

Hii ndiyo tabia yake ya asili. Naam, na ni tabia za watoto wengi wa umri wake, katika mambo kama hayo lazima mtiani mikimikiki.

Lakini tangu aondoke dada wa kazi aliyemlea tangu akiwa mchanga na kuja dada wa kazi mwingine, tabia ya mtoto wako imebadilika sana. Amekuwa akila chakula chote anachopewa na wakati mwingine kwa kujilazimisha mpaka anafikia kujitapikia na pia kila anapokatazwa jambo na dada huyo anasikia na kuacha.

Kama mzazi, unashangazwa kidogo na mabadiliko haya, unafurahia hali hii ya sasa hasa unapoona mtoto wako sasa anakula vizuri na ameacha ile tabia yake ya kukataa kula. Kimoyo moyo unamsifu dada huyu mpya kwamba anajua kukaa na mtoto.

Inapotokea umeshinda nyumbani na kuamua kumlisha mtoto wako wewe mwenyewe, unagundua kuwa bado analeta 'mchezo wake' wa kukataa kula hasa kama dada hayupo karibu naye. Kwa sababu huyo, unamwambia; "ngoja nimuite dada akulishe", na ghafla mtoto anaamua kula.

Kwako kama mzazi unayemtakia mwanao afya njema na shine stahiki, jambo hili la dada 'kumdhibiti' mtoto wako katika suala la kula na kuacha mchezo mchezo linakufurahisha sana. Unashukuru sana kumpata dada wa aina hiyo.

Ni kweli, suala la mtoto kula chakula chake bila kusumbua ni jambo zuri sana. Lishe yake ni muhimu sana kwa makuzi yake. Lakini je, umetulia na kuchunguza hali anayoonyesha mtoto wako wakati akipewa chakula na dada huyu?

Ukitulia na kuangalia 'picha' nzima ya 'kulishana' chakula baina ya dada na mtoto wako, unaweza ukagundua jambo la kustusha! Ni kwamba mtoto wako hali chakula kwa furaha, bali anakula huku akiwa ametawaliwa na hofu kubwa!

Ndio ametawaliwa na hofu haswaaa! Utajiuliza, nini kinachomfanya mtoto wako awe na hofu hii? Jibu ni ukali wa dada.

Katika tafiti nyingi zilizofanywa na wataalamu wa saikolojia juu ya athari za woga na kutojiamini kwa watu wazima, hasa wale waliotoka katika familia za kipato cha kati, imebainika kuwa hali hiyo imetokana na watoto hao kunyanyaswa na madada wa nyumbani wakati wakiwa wadogo kati ya umri wa miaka 3 hadi 5.

Unyanyasaji mkubwa unaotajwa na tafiti hizo, ni ule wa ukatili wa kupigwa au kufinywa na wadada wa kazi hasa kwa watoto wenye usumbufu wa kukataa kula au utukutu wa kitoto unaosababisha kero kwa watu wanaowaangalia.

Na moja ya dalili kwamba mtoto anapitia madhira hayo, ni kuonyesha mabadiliko ya tabia kama kuamua kumaliza chakula anachopewa na dada wakazi au kufanya jambo lolote analoamrishwa pindi anapotishiwa kuwa atafanyishwa na dada wa kazi.

Inawezekana kuwa dada wa kazi aliye nyumbani kwako hana tabia hizo za ukatili na amemfanya mtoto wako kupenda kula na kuacha utundu kwa kumuonyesha mapenzi tu, lakini ni vizuri mzazi pia ukachunguza mabadiliko ya tabia za asili za utoto kwa mtoto wako ili ujue nini kimembadilisha.

## QUIZ

NA KHAMIS KIDAGO 0657 207168

**LE QUIZ**
**•Oanisha maneno kutoka kifungu A na yale ya kifungu B kwa mujibu wa jinsi yanavyoendana (kijinsia).**

**A**


- Beau
- Blanc
- Bon
- Faux
- Fous
- Frais
- Long
- Nouveaux
- Roux
- Vieux
- Gentil
- Doux
- Jaloux
- Gros

**B**


- Nouvelle
- Vieille
- Jalouse
- Belle
- Blanche
- Gentille
- Grosse
- Rousse
- Bonne
- Folle
- Douce
- Fausse
- Longue
- Fraîche

## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA



Alichokifanya daktari

WEWE Unafahamu nani anakupenda zaidi? Sikia maongezi haya mke na mume.

MKE: Mume wangu naomba dawa zangu nimeze

**MUME:** Hizi hapa na haya maji ya kumezea

**MKE:** Karibu tumeze basi mume wangu

**MUME**: Mmmh, kwani ulisikia mi naumwa?

**MKE:** Si uliahidi tutashirikiana kwa kila jambo jamani

**MME**: Sio kwa hilo, kama hutaki niache

SWALI
Ziwa Rukwa linapatikana mkoa gani?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Mume hataki nimpikie hadi arudipo usiku wa manane!

MSOMAJI wangu, karibu tena kwenye safu hii tudadavue yanayojiri kwenye familia zetu. Usione watu wanaonekana barabarani, ofisini au kwenye biashara wamechangamka, huko majumbani mwao siyo shwari. Wengi wanavumilia hadi wanasema basi, Mungu tu asaidie.

Mama mmoja alikuwa anaombewa kanisani. Wakati anapatiwa huduma hiyo ikagundulika kuwa alikuwa amejawa na roho ya uchungu kutokana na vituko anavyofanyiwa na mume wake pasipo sababu za msingi. Yaani anampa masharti ambayo hata mtu mwenye akili timamu akiyasikia anabakia mdomo wazi.

Msomaji wangu, kabla sijaendelea, hebu tuone uchungu ni kitu gani. Uchungu ni mlundikano wa vitu vibaya vilivyowahi kutokea au vilivyotunzwa kwenye nafsi ya mtu. Kwa mfano, kufilisika, ugonjwa wa muda mrefu, kufiwa na mpenzi wako, manyanyaso ya kila siku.

Pia kutengwa, kufiwa na mume, mke au wazazi wako wakati bado ulikuwa ukiwahitaji sana. Vile vile kushindwa kusamehe kwa muda mrefu. Hata Mungu anasema katika neno lake: "Muwe na hasira, ila msitende dhambi, jua lisichwe, na uchungu wenu bado haujawatoka."

Naam. Mama yule alipoulizwa ni kwanini amejawa na uchungu na kushauriwa kwamba akiwa na uchungu kwenye nafsi, tayari anakuwa amemfunguliwa mlango mkubwa shetani ili amtese, akasema;-

"Lipo jambo ambalo limekuwa likinitesa kwa muda mrefu. Mume wangu tangu amenioa miaka miwili sasa, amekuwa ananipa sharti kwamba chakula atakachokula ni lazima nikipike muda ule anaorudi iwe ni mchana au usiku. Naumia zaidi pale anaporudi nyumbani usiku wa manane. Mara nyingi hurudi usiku".

Msomaji wangu, bila shaka umemsikia mpendwa wetu huyu. Hakika alikuwa katika wakati mgumu. Fikiria mume huyu anarudi saa nane za usiku, ndipo mama aanze kukaanga vitunguu na viungo vingine kuandaa chakula wakati watu wengine wamezama kwenye usingizi. Kama siyo maagano ya kishetani ni kitu gani? Nikawaza!

Mara nyingi, mtu mwenye roho ya uchungu, mara zote huwa mpweke, hana furaha, hajikubali na pia huwa mtu mwenye wasiwasi. Mama yule nilivyomuona afya yake ilikuwa dhaifu, pengine pia kutokana na kukosa usingizi mara nyingi hivyo kuwa mchovu.

Mungu hakufanya kosa katika siku ya kwanza ya uumbaji pale alipotenga nuru na giza, akaiita nuru mchana na giza akaliita usiku. Ikawa jioni, ikawa usiku. Wakati wa mchana watu huwa katika pilikapilika mbalimbali za kujitafutia kipato cha maisha, wakati usiku tunapaswa kulala. Labla tu kwa baadhi ya watu wanaofanya kazi za shifti viwandani na kadhalika.

Tabia hii ya baadhi ya wanaume kurejea nyumbani usiku mwingi, imekuwa ni changamoto kwa wanawake wengi hasa wale wanaoangukia kwa wanaume wanywaji pombe kupita kiasi.Pamoja na kwamba wanawaumiza kifikra na kiafya, lakini wao huwa wakali kana kwamba hiyo ni sheria ya kifamilia.

Lakini pia wapo kinamama wanaojitambua huwa hawakubaliani na sharti kama hilo, eti apikiwe pindi arudipo usiku? Wengi huandaa chakula na kuweka kwenye vyombo vya kuhifadhi joto au kupasha moto kama kimepoa. Lakini siyo aanze kukata nyanya, vitunguu, tena usiku kama mama ninayemjadili.

Visheria hivyo vya kifamilia vimesababisha matatizo mbalimbali, mfano hilo la kusababisha uchungu kwa mmoja wa wanandoa. Wanaume wengine hawataki wake zao wafanye kazi iwe kuajiriwa au kujiajiri kwa kisingizio watapata vishawishi na kuingia kwenye mahusiano ya nje ya ndoa. Kumbe hata kama ukimzuia, na endapo ana tabia hiyo, hawezi kuacha. Uaminifu ni jambo muhimu la kufundishana ili maisha yawe na baraka toka kwa Mwenyezi Mungu.

Ni muhimu kinababa watambue kwamba mwanamke anayo majukumu mengi ndani ya familia na hata nje kwa wale wanaofanya kazi ofisini na biashara, Siyo jambo jema kutoa masharti ambayo ni adhabu kwa wenzi wao. Kila mmoja amthamini na kumjali mwenzake kwa upendo ambao ni tunu toka kwa Mwenyezi Mungu.

***Mpenzi msomaji, kwa leo niishie hapa. Je, unacho kisa ungependa tujadili pamoja? Ukiwa tayari tuma kupitia 0715268581. Namba hii pia ipo WhatsApp. Tukutane wiki ijayo.***

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Uchaguzi Mkuu umekwisha tutibu majeraha yaliyojitokeza

UCHAGUZI umekwisha na tayari kwa mujibu wa sheria za Tanzania, baada ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), kutangaza mshindi kwa wingi wa kura, ndiyo inakuwa mchakato wa kupata viongozi wa nchi umekwisha.

Tayari Novemba 2, mwaka huu, Dk. Hussein Ali Mwinyi, aliapishwa kuwa Rais wa nane wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ya Zanzibar.

Novemba 5, mwaka huu, Rais John Magufuli (pichani), aliapishwa kuendelea kuwa Rais wa awamu ya tano Tanzania, ikiwa ni kipindi cha pili baada ya cha kwanza kuanza mwaka 2015.

Kabla ya uchaguzi huo, yalijitokeza mambo mengi ambayo yalionekana wakati wa kura za maoni, watu wanne walifariki dunia, wengi kujeruhiwa na wengine wako jela na mahabusu kwa makosa na tuhuma mbalimbali.

Baadaye wagombea ubunge 28 na udiwani 870 wa vyama vya upinzani walizuiwa kugombea kwa kile kilichoelezwa ni kukosea kujaza fomu za kuomba nafasi hizo na pingamizi lililowekwa na wagombea wa vyama vingine.

Ulipofika wakati wa kampeni wiki mbili za awali, hali ilikuwa shari hadi ilipotokea purukushani baina ya polisi na wafuasi wa ACT-Wazalendo katika Visiwa vya Pemba na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kwa Tanzania Bara. Katika purukushani hizo, kuna waliojeruhiwa na wengine kukamatwa kwa kile kilichoelezwa ni kutenda makosa mbalimbali.

Siku chache kabla ya uchaguzi, vyama vya upinzani vilipaza sauti kuhusu mawakala wao katika vituo vya kura kiasi cha NEC kuongeza muda kuruhusu kuapishwa kwao.

Siku ya uchaguzi mkuu baadhi ya mawakala walilalamikia kunyimwa kuingia kwenye vituo vya kupiga kura, kubadilishiwa vituo na hadi wanavipata tayari kura zilishapigwa kwa kiasi kikubwa.


Wakati wa kupiga kura kulikuwa na malalamiko yaliyotolewa na baadhi ya vyama vya upinzani vikidai kuwapo kwa rafu nyingi, ikiwamo kura zilizokwishapigwa ambazo zilibebwa na watu mbalimbali.

Katika video zilizosambaa mitandaoni zilionyesha kura zilizokamatwa na polisi na wafuasi wa vyama vya upinzani, ambao baadaye walieleza kutiridhishwa na kilichofanyika.

Pia baadhi ya viongozi wa vyama vya upinzani walikamatwa kwa makosa mbalimbali, na wananchi wengine huku Visiwani Pemba kukiwa na waliodaiwa kujeruhiwa kwa risasi.

Yote haya yalitokea katika mchakato wa kidemokrasia kuweka viongozi madarakani ambao wana wajibu wa kuwatumikia wananchi kwa miaka mitano ijayo, kutokana na kile walichokiahidi.

> **"Siku ya uchaguzi mkuu baadhi ya mawakala walilalamikia kunyimwa kuingia kwenye vituo vya kupiga kura, kubadilishiwa vituo na hadi wanavipata tayari kura zilishapigwa kwa kiasi kikubwa.**



Mwisho wa yote ni maendeleo ya wananchi, Mtanzania anataka kuona maisha yake yakibadilika, rasilimaliza taifa zinatumika kwa wote bila kujali itikadi, rangi, dini na eneo wanalotokea.

Sasa pande zote kuna viongozi wa kitaifa ambao sasa wanajukumu la kushughulikiwa malalamiko na kujenga taifa moja katika kuwa za maridhiano ya pamoja, ili kuwa taifa moja na kumaliza majeraha ya uchaguzi.

Majeraha yanaanzia ndani ya vyama vyenyewe kuna walioshinda kura za maoni na kukatwa, kuna walioshindwa kwa kuwa hawakuwa na fedha na kuna walioshindwa kutokana na kupigwa vita na viongozi wa vyama vyao.

Majeraha mengine yalizalishwa kwa watu kupoteza maisha, kujeruhiwa, kufungulia kesi mbalimbali na mwenendo mzima wa uchaguzi ambao kwa waliokuwa uwanjani wanasema kulikuwa na mbigiri ambazo zilisababisha wachezaji kutofanya vizuri.

Yote haya yakiachwa na kuishi mioyoni mwa watu taifa halitabaki pamoja, yawezekana kwa nje likaonekana ni taifa moja lakini kukawa na matendo ya chini kwa chini au mtu na mtu ambayo yataumiza wengi pasipo kujua.

Kwa wakati huu haitakiwi kuwapo wanaopendwa na kuchukiwa, kama ambavyo imesemwa na iko hivyo kwamba maendeleo hayana vyama basi ni wakati muafaka wa kufanyakazi kwa misingi ya maendeleo ya taifa la Tanzania.

Pia, kufanyia kazi malalamiko yote yaliyoibuliwa kiasi cha kuziamsha Jumuiya za kimataifa ambazo kwa nyakati tofauti zimetoa kauli juu ya uchaguzi huo.

Tanzania ilisifiwa kama kisiwa cha amani kiasi cha wengi kuja kijifunza, ilisaidia nchi nyingi kukombolewa dhidi ya mikono ya mkoloni, mara kadhaa tumekuwa wapatanishi kwa nchi zenye machafuko mathalani Kenya, sifa hiyo inapaswa kulindwa na kuenziwa siku zote, ili jina nzuri la Tanzania

***Mungu ibariki Tanzania***

***Kwa maoni/ushauri salomekitomari33@gmail.com***


# HARUSI











Ilikuwa harusi ya kufana kati ya Said Kipeshana na Mwamvita Sama, iliyofungwa Oktoba 29 huko Ukonga Kipunguni B, jijini Dar es Salaam na kufuatiwa na sherehe ya aina yake iliyofanyika ukumbi wa Quality Centre.



# MITINDO









## 'SWAHILI FASHION WEEK 2020'

# Inathaminisha mavazi halisi ya Kiafrika

UNAWEZA kusema Swahili Fashion ni jukwaa la kipekee la maonyesho ya mavazi linalotoa picha halisi ya watu wa Afrika Mashariki na Kati.

Mwaka huu maonyesho hayo ya mavazi yamepangwa kufanyika jijini Dar es Salaam kwa siku tatu kuanzia Desemba 4, mwaka huu.

Mwandaaji wa maonyesho hayo yanayofahamika kama "Swahili Fashion Week & awards", Mustafa Hassanali, amesema jumla ya wabunifu 45 kutoka sehemu mbalimbali duniani watapata nafasi ya kuonyesha mavazi yao.

Licha ya kuwapo vikwazo mbalimbali ikiwamo ugonjwa wa Covid-19, wabunifu hao pamoja na wanamitindo watapanda jukwaani kunadi kazi zao ambazo zina ladha ya Kiafrika zaidi.

"Lengo la kuendeleza tasnia ya ubunifu Afrika bado linabaki mstari wa mbele, kwa kupitia jukwaa hili Watumiaji wa bidhaa wataona thamani ya bidhaa za ubunifu za Afrika," Amsema Assanali.

Maonyesho hayo ya mavazi yataweza kuonyesha dhana halisi ya kutengeneza bidhaa zenye hadhi ya kimataifa kwa misingi ya Kiafrika.

AmEsema maonyesho hayo yanayofanyika kwa mara 13 sasa, yataendelea kuwa kioo kwa mavazi ya Kiafrika na kuwatangaza wabunifu wa Kitanzania Kimataifa.

UREMBO









'CONCEALER'

# Kipodozi kinachompa ujana mwanamke

UREMBO wa sura ni jambo la kuzingatiwa kwa kila Mwanamke ili kumfanya azidi kupendeza na kumuongezea hali ya kujiamini.

Katika kufanya sura iwe ya kuvutia, kuna aina mbalimbali ya vipodozi unaweza kutumia ikiwamo ulaji wa vyakula vya asili na matunda.

Lakini leo itazungumzia aina moja ya kipodozi kinachoitwa 'Concealer' ambacho kazi yake ni kuficha madoa, mikunjo na mabaka usoni.

Kipodozi hiki kipo sawa na 'Foundation' lakini tofauti yake ni Concealer ina weza kutumika peke yake bila kupaka kitu usoni. Concealer zipo za rangi mbalimbali kulingana na aina ya ngozi ya mtu husika, zipo zile zinazong'aa zaidi na zile za rangi ya kufifia.

Lakini unashauriwa ukatumia inayo endana na rangi yako ili upate muonekano wa kiasili.

**1) Stick Concealer'**

Hii inapatikana katika kikopo kama cha lipstick' lakini Concealer hutumika kupaka kwenye ngozi kama vile poda au foundation.

Aina hii hutumika sehemu ya sura, ni nzuri ukitumia mkono kupaka. Hutumika pia chini ya macho, ngozi iliyoathiriaka na vipele au kufifia kutokana na magonjwa ya ngozi.

**2: Pencil Concealer**

Aina hii ya Concealer inafanana na penseli au wanja, hutumika kuchorea sehemu iliyo athirika, kisha tumia blashi kusawazisha eneo husika.

**3: Cream Concealer**

Hutumia kupakaa uso mzima na una weza kupaka ukitumia vidole au brashi. Nzuri kutumika chini ya macho au sehemu yoyote iliyofifia. Ni rahisi kutumia hata ukiwa na haraka.

Kwa msaada wa mtandao

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Kula nyanya chungu upate faida kiafya



NYANYA chungu, maarufu kwa jina la ngogwe ni aina ya mboga yenye faida mbalimbali kwenye mwili wa binadamu.

Kuna aina mbili za nyanya chungu, zipo zile zilizo chungu na zile za baridi ambazo hupendwa na watu wengi.

Nyanya chungu hutumiwa na wengi kama mboga au kiungo kimoja wapo katika kunogesha mboga.

Kwa wachache wanaofahamu faida za nyanya chungu kiafya hutumia kama mlo kwa kupika kama mchemsho wa supu au kuweka kwenye kila mboga.

Nyanya chungu husababisha mboga kuwa na ladha na harufu ya aina yake.

**MAPISHI YAKE**

Nyanya chungu unaweza kuzichemsha chupuchupu na kula kama supu.

Pia unaweza kuzipika kwa kuchanganya na bamia na majani ya



maboga na kuwa mlenda.

Pia unaweza kuzitumia kwa kuzipika zenyewe na bamia na kuwa mlenda.

Pishi lingine la nyanya chungu ni kiungo cha mboga kwa kuchanganya kwenye nyama, samaki, dagaa na mboga za majani kama kisamvu.

Nyanya chungu pia zinaweza kupikwa kwa kuchanganywa kwenye pishi la ndizi.

**FAIDA ZAKE**

Nyanya chungu zinafaida mbalimbali kwenye mwili wa binadamu, ambazo ni pamoja na kujenga na kuimarisha afya ya mlaji.


Nyanya chungu ipo kwenye kundi la mbogamboga zenye virutubisho vingi ikiwemo vitamin A, B, na C ambazo zote kwa pamoja hufanya kazi ya kuobresha afya ya mwili.

Nyanya chungu pia husaidia kuimarisha kinga ya mwilli na kumsaidia mlaji.

Pia humsaidia mlaji kuepukana na magonjwa ya mara kwa mara kama homa na mafua.

# MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Athari udongo mfinyanzi katika ujenzi wa nyumba



MAKALA ya leo tunaangalia madhara yatokanayo na kujenga nyumba katika udongo wenye mfinyanzi.

Msanifu Majengo, Alex Katola, anasema unapofanya ujenzi jambo la kwanza kuangalia ni aina ya udogo uliopo kwenye eneo lako la ujenzi. Anasema utambuzi huo utakusaidia kuepuka matatizo ya baadae katika nyumba yako na anashauri kwamba kama hujui kutambua aina ya udongo katika eneo lako ni vema ukawasiliana na mtaalam.

"Udongo wa mfinyanzi una tabia ya kusinyaa na kutanuka, tabia hii husababisha madhara endapo utajenga katika udongo wa aina hii bila kuzingatia kanuni za ujenzi kwenye eneo la mfinyanzi," anasema Katola.

"Njia hii rahisi ya kutambua udongo wa mfinyanzi ni kuangalia alama za mipasuko kwenye ardhi ambayo hutokea hasa katika kipindi cha kiangazi ambapo udongo huu husinyaa sana na kutokuwa na unyevunyevu."

Anasema miongoni mwa athari ambazo hutokea kwa kujenga nyumba yako kwenye udongo huo ni pamoja na kusababisha nyufa na mipasuko katika maeneo mbalimbali ya nyumba ikiwamo kwenye msingi, kuta, nguzo, na sakafu.

Katola anashauri kwamba unapojenga nyumba katika eneo la udongo wa mfinyanzi mambo unayotakiwa kufanya ni pamoja na kuondoa kabisa udongo huo eneo unalojenga msingi wako.

"Kwa kutumia mtaalam wa ujenzi utashauriwa namna ya kutoa udongo uliopo na kuweka mwingine kwa kiasi kinachotakiwa,"alisema Katola.

Pia anasema kwamba unaweza kujenga nyumba yako katika udongo huo wa mfinyanzi bila kuuondoa hususani katika kipindi cha kiangazi.

"Unaweza kujenga nyumba yako bila kuondoa udongo wa mfinyanzi katika kipindi cha kiangazi na ukimaliza unatakiwa kuweka miundombinu ambayo utahakikisha maji hayafiki kwenye msingi wa nyumba yako,"anasema Katola.

## MPANGILIO

### Dondoo ya kupanda mchaichai kuzunguka nyumba kuipendezesha

**1:** Chagua miche bora ya mchaichai na kisha kata majani yake kwa juu

**2:** Andaa mashimo pembeni ya nyumba ukiacha nafasi ya mita moja kutoka ukutani


**3:** Mwagilia maji kila siku asubuhi na jioni.

**4:** Kama udongo umechoka, ongeza mbolea ili kusaidia kukua kwa haraka.

**5:** Mimea ikikua chuma majani kwa kukata chini kwenye shina, isikate kwa mikono unaweza kusababisha mchaichai kukauka haraka.



## KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2020
SMS - 0621 412 879
Haya Bwana Wewe! Uchaguzi Umekwisha Na mshindi Ameapishwa, Wewe Ulikuwa Wapi TOKA SIKU YA KURA?
Nikikutajia Nilipokuwa Hayatakuwa MAKUBWA?
Dawa ya Kupambana Na 'STROKU' ya kukosa JIMBO ni kupiga tizi na Suti za BUNGE Lilopita...
Kwa Hiyo Unanishauri Niwe mpore NIKUBALI
Tena Sana! Ukiona Kura HAZIKUTOSHA huwezi kuzipeleka kwa Fundi zika-Ongezwe Ukubwa
JUKWAANI
BABA MKWE! Mbona Unaghadhabu Kama wewe Ndiye Mgombea Uliye-angushwa?
Ushanitia Aibu... SHIKA CHINI KWANZA kisha Unielezee kwanini UMEBWAGWA?
Misukosuko Yote Hii... Lakini Vitambi Bado VIMETUGANDA!
KITAMBI CHA SHIDA, NI RAFIKI WA KWELI...
Mtaalamu... Moyo Wangu Hautaki kuamini MATOKEO ya Kura NILIZOPATA 'Nifanyeje?'
Kalete Jogoo na mayai Manne Mchele nazi Tatu iriki na Giligilani Na Mkaa Kiroba. NIUTAMBIKIE
MGANGA
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...KAMA UNAJUA, SHULE ULIFUATA NINI?...

HABARI KIMATAIFA

# Joe Biden aelekea kupata ushindi awataka Wamarekani kukaa tayari

**WASHINGTON, Marekani**

MGOMBEA Urais kwa tiketi ya chama cha Democratic, Joe Biden, amezungumza na Wamarekani na kutaja tena vipaumbele vyake katika kipindi hiki akiashiria kupata ushindi wa urais.

Licha ya kwamba kuhesabu kura hakujakamilika, Biden alisema jana kuwa hatua ya ushindi inayoashiria inafungua njia ya kukabiliana na corona, vitendo vya ubaguzi na mabadiliko ya tabia nchi na mambo mengine muhimu.

Mgombea huyo aliyasema hayo, wakati kukiwa na dalili kubwa ushindi katika majimbo muhimu, huku mpinzani wake, Donald Trump, akiendelea kulalamikia kuchezewa rafu na kutaka majimbo hayo kusimamisha mchakato wa kuhesabu kura.

Hadi jana, Biden, alikuwa akihitaji kura sita za wajumbe wa majimbo ili kumwezesha kufikia 270, idadi inayohitajika kumuingiza Ikulu.

Katika jimbo la Arizona, ambako asilimia 94 za kura zilizohesabiwa, Biden alikuwa na asilimia 49.9 na Trump asilimia 48.6.

Jimbo la Pennsylavania wamehesabu kura kwa asilimia 96 ya, Trump alipata asilimia 49.2 na Biden 49.5.

Katika jimbo muhimu la Georgia, kura zilizohesabiwa hadi siku hiyo, zilikuwa ni asilimia 99 ambapo Biden alikuwa na asilimia 49.5 na Trump asilimia 49.4.

"North Carolina tayari kura zilikuwa zimehesabiwa kwa asilimia 98, Trump alikuwa na asilimia 50.0 na Biden asilimia 48.6, huku jimbo la Nevada lenye asilimia 93 za kura zilizohesabiwa, Trump alikuwa na asilimia 48.0 na Biden asilimia 49.8."

Kwa upande wa Pennsylavania, chama cha Republican kimeitaka Mahakama Kuu kuwasimamisha maofisa wa uchaguzi, kusimamisha kura ambazo ziliwasilishwa katika maeneo ya kuhesabu kura baada ya kupita siku ya uchaguzi.

Kiongozi mwenye dhamana na masuala ya nje wa jimbo hilo, maofisa wote wa vituo vya kuhesabu kura katika jimbo hilo wameamrishwa kutimiza takwa hilo, ingawa kwa upande wa Republican walisema hakujawa na uhakika wa jambo hilo kutekelezwa na maofisa wote.

Katika matukio mawili tofauti, Mahakama Kuu ya Marekani imekataa kuingiliwa, kufuata maombi ya Republican ya kugeuza uamuzi.

Timu ya kampeni ya Donald Trump ipo katika mchakato wa kushiriki makabiliano ya kisheria, lengo likiwa ni uhalali kuwasili baada ya uchaguzi kwa kura zilizopigwa katika jimbo la Pennyslavania.

Takwa hilo la kisheria la Republican, linahusu rundo la kura zilizopigwa kwa njia ya posta, kutoka upande wa Pennyslavania, ambalo linajumuisha mji wa pili kwa ukubwa wa Pittsburgh.

Watu wawili wenye kujihami na silaha wametiwa mbaroni, karibu na eneo ambalo kunahesabiwa kura ambazo zitaamua nani atakuwa rais wa taifa hilo kati ya Trump na Biden.

Kwa mujibu wa polisi, waliotiwa mbaroni ni Joushua Macias (42) na Antonia LaMotta (51) ambao wanatajwa kutoka maeneo ya Virginia na kwamba hawakuwa na kibali cha kubeba silaha hizo zilizokuwa zimesheheni risasi.

**DW**



Mgombea wa urais wa Marekani kupitia chama cha Democratic, Joe Biden, akizungumza na wafuasi wake jana wakati akielekea kupata ushindi wa nafasi hiyo. Kushoto ni mgombea mwenza, Kamala Harris. **(PICHA: DW)**

# Kiongozi wa upinzani akamtwa

KIONGOZI wa upinzani nchini Ivory Coast, Pascal Affi N'Guessan, amekamatwa akituhumiwa kuunda serikali yake.

N'Guessan, aliunda serikali hiyo baada ya ushindi wa rais Alassane Quattara kwenye uchaguzi uliomalizika.

Taarifa ya kukamatwa kwa kiongozi huyo wa upinzani ambaye alikuwa waziri mkuu wa nchi hiyo wakati wa enzi ya Laurent Gbagbo, kuanzia mwaka 2000 hadi 2003, ilitolewa na mkewe kwa pamoja na msemaji wa kiongozi huyo.

Waendesha mashtaka nchini humo wamefungua kesi inayohusiana na ugaidi dhidi ya viongozi kadhaa wa upinzani ambao walisusia uchaguzi uliofanyika Oktoba 31, mwaka huu.

Wapinzani wanadai Quattara, alikiuka katiba kwa kugombea muhula wa tatu.

**DW**

# Raia wa Misri wachagua wabunge

**CAIRO, Misri**

WANANCHI wa Misri, jana walipiga kura kuwachagua wabunge katika duru ya pili na wa mwisho wa kuwapata viongozi hao. Vituo vya kupigia kura vilifunguliwa saa tatu asubuhi katika majimbo 13 kati ya majimbo 27 yaliyopo nchini humo. Majimbo yaliyopata nafasi ya kupiga kura ni mji mkuu wa Cairo na sehemu ya kaskazini ya Rasi ya Sinai.

Kulingana na taarifa kutoka Ikulu, Rais Abdel-Fatah El-Sissi, alishiriki katika zoezi hilo siku ya Jumatano. Zaidi ya raia milioni 31 wana haki ya kupiga kura katika duru hiyo ya pili. Ingawa idadi ndogo ya watu ilijitokeza kupiga kura katika duru ya kwanza.

Wakosoaji walisema bunge jipya halitokuwa na tofauti na lilopita. Wagombea kutoka upande wa vyama vinavyomuunga mkono El-Sissi, wanatarajiwa kushinda kwa wingi kwenye bunge hilo lenye viti 59.

**DW.**

## Wabunge waiondoa serikali ya Tigray

**ADIS ABABA, Ethiopia**

WABUNGE wa Ethiopia, wamepiga kura ya kuiondoa madarakani serikali ya jimbo la Tigray na kuidhinisha kuundwa serikali ya mpito.

Hatua hiyo inakuja siku chache tangu serikali kuu inayoongozwa na Waziri Mkuu, Abiy Ahmed, kutangaza kuanzisha operesheni ya kijeshi katika eneo hilo.

Mapigano yalianza siku ya Jumatano kati ya vikosi vya serikali ya shirikisho na wanamgambo kutoka jimbo hilo, baada ya Abiy kutuma vikosi vya kijeshi katika eneo hilo. Waziri Mkuu huyo alikishutumu chama cha Ukombozi wa Watu wa Tigray (TPLF), kwa kufanya mashambulizi katika kambi ya jeshi la shirikisho kwa lengo la kuiba vifaa vya kivita.

**DW.**

## Rais wa Belarus awekewa vikwazo

**BRUSSELS, Ubeligiji**

UMOJA wa Ulaya (EU), umemuwekea vikwazo Rais wa Belarus, na viongozi wengine 14 wakihusishwa na vitendo vya ukandamizaji wa raia.

Kiongozi hiyo, aliamuru kutumia nguvu kubwa kudhibiti maandamano ya kupinga uchaguzi wa rais uliofanyika mwezi Agosti mwaka huu.

Umoja huo, ulisema katika taarifa yake kwamba, Rais Alexander Lukashenko, mtoto wake pamoja na mshauri wake wa usalama wa taifa, Viktor Lukashenko, wamewekwa kwenye orodha ya vikwazo hivyo.

Watu hao watakabiliwa na vikwazo vya kusafiri ndani ya mataifa ya Ulaya na kuzuiwa mali zao.

Aidha raia wote wa Ulaya pamoja na kampuni za kiabiashara hawaruhusiwi kuwapata mikopo.

Tangu mwezi Agosti watu wanaendelea kuandamana nchini Belarus, na zaidi ya watu 15,000 wamekamatwa na polisi.

**DW.**

## MAKALA

# Kuwa kondakta uwe kiongozi bora



Na Magabilo Masambu

BASI watoza ushuru wote na wenye dhambi walikuwa wakimkaribia wamsikilize. Mafarisayo na waandishi wakanug'unika wakisema mtu huyu huwakaribisha wenye dhambi tena hula nao.

Akawaambia mfano huu akisema: "Ni nani kwenu mwenye kondoo mia akipotewa na mmojawapo asiyewaacha wale tisini na kenda nyikania ende akamtafute yule aliyepotea hata amwone?

Naye akiisha kumwona humweka mabegani pake akifurahi na afikapo nyumbani kwake huwaita rafiki na majirani zake akawaambia furahini pamoja name kwakuwa nimekwisha kumpata kondoo wangu aliyepotea."

Tunaweza kuwa mashahidi majumbani mwetu kwamba hata shilingi moja kwenye shilingi mia ikidondoka ndani ya nyumba gizani, lazima tuwashe taa kuitafuta bila kujali ni fedha kidogo kiasi gani kwa sababu mia hukamilishwa na shilingi moja.

Wote tunasafiri kwenye mabasi, daladala na vyombo vingine vya usafiri. Tuzungumze kuhusu daladala ambazo wengi tunazitumia kama usafiri wa umma, tumekuwa tukishuhudia tabia za makondakta utafikiri wamepata mafunzo chuo kimoja kuanzia uvaaji pamoja na tabia zao.

Tabia moja waliyonayo ambayo ni nzuri kama wangaliitumia viongozi wetu na kuwafanya wawe viongozi bora kabisa, ni tabia ya kuthamini aliye nje ya daladala zaidi kuliko aliyekwisha kuingia ndani.

Kondakta huwa ana kituo kila mahali cha kubeba abiria wanaoingia kwenye daladala.

Anaweza kusimama hata kwenye reli! Lakini wakati wa kushusha huwa anashusha mahali penye kituo maalumu tu! Na mara zote awapo kwenye daladala, kichwa chake hutoa nje kuangalia wanaotaka kuingia kuliko kusikiliza sauti za wale wanaotaka kushuka kwenye kituo.

Maana yake ni kwamba iwapo utapanda kwenye daladala ukasahau kutaja kituo chako basi ni rahisi zaidi kupitilizwa kwa sababu kondakta huwa hana mpango na wewe tena bali ana mpango na walio nje.

Tumemaliza uchaguzi mkuu kwa vyovyote ulivyoonekana sitaki kusema sana dhidi ya uchaguzi wenyewe lakini ni juu ya viongozi waliopatikana.

Kiongozi yeyote aliyepatikana kabla ya wananchi kuamini kwamba hawakumchagua au walimchagua jukumu la kiongozi aliyepatikana wazo lake la kwanza analotakiwa kuwa nalo ni yeye kufikiri kwamba amechaguliwa na wananchi wote.

Kama ni Diwani kwenye kata yake, kama ni Mbunge kwenye jimbo lake, kama ni Rais ni nchi nzima. Hili litamfanya kiongozi wa namna hii asitoe huduma kwa kubagua kwa kudhani kwamba wapo ambao hawakumchagua na akifanya hivyo, anajiwekea ugumu kwa uchaguzi ujao.

Ushauri wangu mkubwa kwa viongozi wote waliopatikana, fanyeni tathmini au kautafiti kadogo muone wapi hamkukubalika zaidi ili nguvu kubwa ya upendo na huduma zielekezwe huko. Sina maana kwamba wale mnaodhani ndiyo waliowachagua msiwape huduma.

Ili kuunganisha na kuponya majeraha ya uchaguzi ni kuwafikiria wale kondoo wachache zaidi kuliko wale tisini na kenda waliowachagua kwa sababu hao tayari wameshakuwa wa kwenu. Kwa hiyo lazima kutafuta wengine zaidi ili kuwaleta pamoja kondoo wote.

Uongozi ni pamoja na kuwaweka watu pamoja ili maendeleo wafanye wao wenyewe kwa ushirikiano na kazi yenu kama viongozi itakuwa kuwahamasisha wafikie malengo yao bila kukokotwa kama watumwa. Tuwe watumishi kuliko kuwa mabwana.

Fedha zinazotumika kufanya maendeleo hutoka kwa wananchi kwa njia ya kodi au njia nyinginezo kwa maana nyingine ni kwamba viongozi kazi kubwa waliyonayo ni kuhakikisha wana usimamizi mzuri wa fedha hizo.

Kwa maana hiyo, hakuna kiongozi atakayeleta maendeleo yetu kwa fedha zake mfukoni bali sisi wenyewe na jambo hili linafanyika kwa usahihi kama tutakuwa wamoja na wenye kufanya kazi hiyo ya kutuweka pamoja ni viongozi.

Nyakati za uchaguzi, kila mtu huwa na chaguo lake na si dhambi kwa mujibu wa sheria zetu, hivyo haitakuwa sahihi kutumia uchaguzi uliopita kuhukumiana bali tuutumie kuungana pamoja na pengine kuanza maandalizi ya uchaguzi ujao wa 2025 ambao maandalizi yake yanafaa kuanza sasa.

Maandalizi hayo si kwa maana ya kuandaa vifaa bali kuwaandaa wapigakura kwa kuwatendea mema yatakayowafanya wakuchague tena awamu ijayo. Kuwa kondakta uwe kiongozi bora, walio wako ni wako tu tafuta wasio wako wawe wako.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Wapenzi walivyopatikana bila simu, meseji



Na Adam Fungamwango

TEKNOLOJIA kwa kiasi kikubwa imebadili utamaduni na mfumo wa maisha. Leo tutazungumzia zaidi teknolojia ya simu za mkononi ambazo zimeleta utamaduni na utaratibu mpya kabisa za maisha, tofauti na ule wa zamani. Mwingine ni hasi na mwingine ni chanya.

Simu za mkononi zilianza kuwapo nchini katikati ya miaka ya 1990, tena zilikuwa chache na wamiliki wake pia huku ikiwa ni gharama kubwa kuimiliki. Kwanza zilikuwa kubwa kama 'radio call' halafu kila teknolojia ilivyozidi kukua, zikawa zinapungua uzito na ukubwa pia.

Angalau watu wengi walianza kumiliki simu kuanzia miaka ya 2000 na kuanzia hapo simu ikawa si anasa tena, bali ni sehemu ya maisha. Baadhi ya watu bila simu sasa hawezi kufanya kitu chochote kile. Hawezi hata kuingiza pesa. Kula yake na kuvaa inategemea simu ya mkononi.

Kipo kizazi ambacho kimeondoka duniani kikiwa hakijatumia kabisa simu za mkononi. Na kuna kizazi ambacho kama chaja ya kobe, chenyewe kimeishi maisha ya bila simu na pia wakati huu wa maisha ya simu za mkononi. Sasa kuna kizazi ambacho chenyewe kimezaliwa kimezikuta simu za mkononi kwa wingi.

Hawa wakisimuliwa maisha ya watu waliokuwa wanaishi bila simu wanashangaa. Wanaona kama ni hadithi za kufikirika hivi. Wanaoamini wanaona kama kizazi hicho kilipata shida sana. Wakati mwingine wanaona kama ni burudani hivi kwa jinsi shida zilivyokuwa zikiwapata baba na kaka zao.

Usiombee sasa ukutane na kizazi ambacho kimeishi maisha yote ya pande mbili. Wao wanapokaa na kuhadhithiana walivyofanya, staili walizotumia na vituko mbalimbali, inakuwa burudani iliyotikisa.

Mume akitaka kumsafirisha mke, mfano kwenda kwao kusalimia, basi ilikuwa lazima ampe nauli ya kwenda, kurudi na fedha ya matumizi. Asipofanya hivyo, hawezi kurudi mpaka atume nauli kwa njia ya posta na ilichukua muda mrefu kufika kwa uchache wiki tatu hivi au zaidi, tena ipitie kwa mtu mwenye sanduku la posta. Akiondoka hawawezi kuwasiliana tena hadi arudi, au yeyote kati yao aandike barua na kuituma posta.

Kwa sasa mume anaweza kumpa nauli tu mke ya kwenda. Halafu wakawa wanawasiliana kama vile wako wote kila siku au kila muda watakaopenda kupigiana simu au kutumiana ujumbe mfupi wa maandishi, maarufu kama meseji. Na mke akitaka kurejea anamwambia tu mumewe, pesa itatumwa kwenye simu siku ile ile ya kurudi na nauli itapatikana na tiketi itakatwa. Wanaweza hata kuwasiliana "umefika wapi?" Hiyo ndiyo teknolojia.

Kukua kwa teknolojia kumerahisisha hata jinsi ya wanaume au vijana kupata wenza wao, ambao mwanzo wanakuwa wapenzi, baadaye wachumba na mwisho wanakuwa wake zao. Kijana wa sasa hana mambo mengi. Ataomba namba ya simu tu ya msichana, biashara imekwisha. Mambo mengine yataenda taratibu hadi yatakaa yenyewe sawa. Watawasiliana na kubembelezana kila siku. Yasipokaa sawa, basi haiku-pangwa iwe.

Yeyote yule anapiga simu kuwa wakutane sehemu fulani, kituo fulani au maeneo fulani. Mwingine hata kama amefika, atampigia mwenzake kujua "umekaa wapi", "uko wapi?", "mbona sikuoni?", "aah basi nimekuona." Ni rahisi sana tofauti na zamani. Sasa hebu sikiliza masahibu waliyokuwa yakiwapata vijana au wanaume wa zamani.

Hakuna namba za simu au simu zenyewe, hivyo anapokutana na msichana ni lazima amkabili uso kwa uso na kumwambia ukweli kuwa anampenda, vinginevyo imekula kwake.

Kuna wakati inashindikana kutokana na mazingira au kuona aibu, hivyo kulikuwa na njia mbadala ambayo ilikuwa ya hatari, kuandika barua na kumpa rafiki yake ampelekee au kumtuma mtoto. Hii wakati mwingine ilijulikana kwa wazazi na walimu, pale barua itakapoangukia mikononi mwa wasiohusika kwa bahati mbaya. Na hata ahadi za kukutana zilifanyika pale wanapokutana wawili. Watapanga kukutana lini na staili fulani ya kufanya ambayo ni wao tu ndio wataifahamu. Ni kwamba kijana atapita nyumbani kwa msichana na kurusha kijiwe juu ya bati ili iwe wito kuwa anapita sasa na yeye atoke. Wakati mwingine mwanamume anapiga hata miluzi au kuimba. Anayejua nini kinatakiwa kufanyika ni msichana tu.

Kuna kuahidiana kukutana siku fulani, sehemu fulani, na saa fulani. Sasa kama msichana hakufika siku hiyo basi hiyo ndiyo inaitwa 'kuachwa solemba'. Ni tofauti na sasa, kabla yeyote hajanyanyua mguu, kama kuna dharura watajulishana. "Siwezi kuja leo, shangazi anaumwa."

Ni faida kwa vijana wa sasa kabla ya kuelekea kwenye ahadi. Wale wa zamani walikuwa hawana faida hiyo, atafika na atapoteza muda na gharama kama msichana hakuja. Hii ni kutokana na kutokuwa na teknolojia ya simu.

Kuna waliokuwa wakishindishwa kwenye vibaraza, chini ya mti, kwenye kona za nyumba za watu na sehemu zingine zinazofanana na hizo. Kuna wengine waliwahi kufurumushwa na nyuki, nyoka, mbwa kutambaliwa na washawasha, kuumwa na nyigu wakiwasubiri wapenzi wao, hasa wale wa vijijini. Hizi zote ni zile hatua ya mwanzo kabisa, kabla ya kijana kwenda kujitambulisha kwa wazazi.

Vijana wa zamani wanasema kuwa ugumu waliokuwa wakiupata wao ndiyo unasababisa hata ndoa zao kudumu, kwa sababu walipata wapenzi, wachumba na wake zao kwa tabu. Kwa njia ngumu na za hatari, zilizohitaji uvumilivu wa hali juu, tofauti na vijana wa sasa ambao wanawapata kirahisi, kwa kurahisiwa kazi na teknolojia ya simu za mkononi.

Sijui kama kuna ukweli au la, lakini ukweli inabaki pale pale kuwa kabla ya teknolojia ya simu za mkononi, aliyekuwa anatafuta msichana ilibidi aache kazi, afanye kazi. Yoyote atakayekusimulia jinsi alivyompata mkewe ni zaidi ya burudani, unaweza kukauka au kuvunjika mbavu kwa kucheka, kwani kila mmoja alikuwa na staili yake, zinazovutia kuzisikiliza.

# HADITHI

WASWAHILI wanasema mshika mawili moja humponyoka, na karamu mbili zilimshinda fisi. Cecilia, msichana mwenye kila sifa ya kuitwa msichana mrembo, anaangukia kwenye mapenzi ya vijana wawili.Mmoja ni fukara na mwingine mwenye uwezo. Kutokana na mwenyewe Sesilia kutokuwa na msimamo wenye kueleweka, anawaingiza vijana hao kwenye chuki na visasi, vilivyoambatana na wivu uliopindukia na kusababisha maafa makubwa. Ni kisa cha kusikitisha, kutisha na kuhuzunisha, lakini chenye elimu kubwa.

# Adui Namba Moja-7

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**




Alimwangalia Zahir akamwona ni mtu mwenye uwezo wake lakini ni mtu anayemhitaji zaidi Cecy kujifurahisha nafsi yake tu bila kujali chochote kinachomhusu.

Hata yeye mwenyewe alishawahi kumwona mara moja tu, tena akiwa na haraka kama mtu anayetaka kwenda kuzima moto.

Anakumbuka jinsi dada yake alimpomtolea povu siku ile kule kwenye Hospitali ya Mwananyamala. Anakumbuka usaliti wote ambao dada yake ameufanya, hivyo kitendo cha kuonekana kujutia, aliona ana haki ya kumsaidia dada yake arejee kwa mwanamume ameyependa na kujali.

Badaka pia aliona atatumika kwenye usuluhishi kwa sababu anaelewana sana na Mashaka. Hata siku ambayo kulitokea tafrani hospitalini, ni yeye ndiye aliyeizima na kumchukua kwenda naye.

Kabla ya hapo ndiye aliyempigia simu Mashaka. Na hata mama yao alipolazwa kwa mara ya pili, alimpigia na kumwarifu pia.

Na hata mama yao Magdalena ameshaanza kumfahamu kwa kumuona mara mbili, ingawa anadhani kuwa anaweza kuwa ni mpenzi wake na si wa Cecy. Ni kwa sababu mara zote mbili wanakuwa wote wawili.

Hayo yote alipoyafikiria alijiona ni mtu muhimu kuongozana na dada yake.

Cecy, baada ya kujipamba alivaa nguo mpya nzuri, zilizomkaa vyema. Lengo ni kuushtua upya moyo wa Mashaka ambao anaona kwa sasa utakuwa amesinyaa.

Akaona haitoshi. Akapika chakula kitamu ambacho Mashaka anakipenda. Ulikuwa wali wa nazi, samaki aina ya kitoga. Aliunga na nazi, akiweka bamia na nyanya chungu. Ni chakula ambacho anakipenda mno.

Alipulizia na marashi ambayo aliwahi kununuliwa naye huko nyuma. Safari ikaanza kwenda nyumbani kwa Mashaka. Ilikwenda kama walivyopanga, kwani walimkuta. Mashaka alikuwa wa kwanza kuwaona wageni wake aliowatarajia, ingawa alikuwa na maswali na mawazo mengi kichwani.

Hata hivyo, kwa jinsi alivyokuwa akiwatazama mtu na dada yake, aliwaona kama wana kitu wamekuja nacho ambacho ni cha kheri na wala si shari.

Mshangao mwingine ni pale baada ya salamu na kuwakaribisha, alikabidhiwa mfuko uliokuwa na chombo cha kuhifadhia chakula na Cecy, tena kwa heshima zote. Kwa mbali alihisi faraja. Lakini bado aliendelea kukumbuka madhila aliyoyapata kwa siku za hivi karibuni.

**"Dunia imenipiga fimbo mwenzako. Mimi kusema kweli nakupenda sana Mashaka. Ila nilidanganywa na ulimwengu, lakini muda ni wakati mzuri. Kuna vitu vingi nilikuwa sivijui, lakini leo nimetambua kuwa penzi lina nguvu kuliko pesa." Aliongea kwa majonzi huku akiwa hamwangalii Mashaka usoni.**

"Mashaka mimi nimekuja." Ilikuwa dakika tatu za ukimya, huku matonge ya wali na minofu ya samaki ikiwa inateketea kwenye tumbo la Mashaka. Hakujua ajibu nini, kwani ni kweli Cecy alikuwa amekuja, lakini nini kimemleta?

"Ndiyo, nakusikiliza." Alisema kwa sauti ya udadisi.

"Kuja kwangu leo hapa, kwanza kabisa naomba niombe samahani kwako kwa yote ambayo nimekutendea, siku ile hospitalini na siku zingine ambazo nimekukosea sana." Cecy alianzisha mada na kunyamaza, kumpa nafasi Mashaka kama ana lolote lile aongee lolote lile.

Mashaka alinyamaza kimya. Hakuonekana kama amekasirika au kufurahi, kukataa msamaha au kukubali. Aliendelea kula taratibu chakula anachokipenda. Hakuna kitu kilichomuogopesha Cecy kama hicho. Hakujua Mashaka yupo upande gani. Atamsamehe au la.

"Dunia imenipiga fimbo mwenzako. Mimi kusema kweli nakupenda sana Mashaka. Ila nilidanganywa na ulimwengu, lakini muda ni wakati mzuri. Kuna vitu vingi nilikuwa sivijui, lakini leo nimetambua kuwa penzi lina nguvu kuliko pesa." Aliongea kwa majonzi huku akiwa hamwangalii Mashaka usoni.

Kama kawaida, Mashaka hakusema chochote.

"Mashaka unamsikia dada lakini?" Badaka alidakia.

"Namsikia, siyo vizuri kumkatisha, mwache tu andelee."

"Mimi ni mwanamke niliyefundwa Mashaka, sitaki kuongea vitu vingi ambavyo nimepitia uvisikie kwa sababu vinaweza kukuchoma moyo, lakini nataka kukwambia tu, wewe ndiwe chaguo langu sahihi. Nimegundua wewe ndiwe mwanamume unayenipenda kwa dhati. Naomba msamaha tuwe kama zamani."

Cecy alishusha pumzi ndefu. Tayari alikuwa ameshaeleza kilicho moyoni mwake. Sasa chochote kitakachotokea alikuwa tayari kukabiliana nacho.

"Nimekuelewa Cecy. Hata mimi nakupenda na nitaendelea kukupenda daima, kwa sababu moyo wangu ulikuchagua wewe pekee. Hata hivyo, nilivunjika moyo pale uliponikataa. Halafu si kunikataa tu, lakini ukanikandika na maneno mabaya. Maneno ya kukatisha tamaa. Unajua yale maneno ni bora uambiwe na mtu mwingine. Lakini siyo unayempenda. Yanauma sana." Mashaka alitoa nyongo.

Sauti aliyokuwa anaongea haikuwa kama mtu anayesimanga au kulaumu. Alikuwa kama analalamika na kuugulia maumivu yaliyo moyoni mwake.

"Jamani Mashaka, najuta, usirudie tena kunikumbusha kilichotokea nyuma."

"Cecy, mimi nakwamba nitaendelea kukupenda. Nimekuelewa ila naomba kwanza nipe wiki moja nitafakari."

"Ina maana bado hujakubali msamaha wangu Mashaka?"

"Hapana, kutafakari maana yake nikae na kumwomba Mungu ili nikikusamehe kusiingie tena kidudu mtu."

Cecy ikawa inakuja, inakataa. Ni kama alikuwa anataka kumwelewa, lakini baadaye anashindwa kumwelewa. Hata hivyo, aliona heri nusu shari kuliko shari kamili. Hata Mashaka angeamua kukataa, asingeweza kumfanya kitu chochote.

"Mashaka rudisha moyo wako, dada anakupenda sana na wewe unampenda. Kwenye mapenzi ya kweli changamoto kama hizi ni lazima zitokee." Badaka naye aliingilia.

"Unafikiri dada yako alivyokuwa ananikataa ningetafuta mwanamke mwingine? Ningekuja kukuoa wewe tu mdogo wake, inatosha, wala nisingeenda mbali." Vilifuatia vicheko kutoka kwa Cecy ambaye alikuwa katika hali ya wasiwasi na kutojiamini muda wote. Ulikuwa mzaha wa Mashaka kwa shemeji yake Badaka. Mara nyingi ni mizaha ya mara kwa mara ambayo hufanyiana.

"Nyinyi wala msiwe na wasiwasi na mimi, kuweni na amani, kila siku niko na nyinyi. Mungu akipenda yataisha tu haya."

INAENDELEA JUMAPILI

## HABARI BURUDANI




# Hajatokea wa kumzuia Harmonize

MKURUGENZI wa lebo ya Konde Gang, anayejulikana kwa jina la Jembe, amesema hakuna mtu wa kumzuia Harmonize, kupata kazi za kimataifa.

Jembe amesema kila kitu kinapangwa na Mungu, hivyo hakuna mtu ambaye anaweza kuzuia kuchukua nafasi yake na kuzuia mambo mazuri ambayo msanii huyo anastahili kupata.

"Hakuna anayeweza Harminize asipate kazi za kimataifa, riziki hupangwa na Mungu na kama akitaka iwe basi huwa, nawashukuru mashabiki wetu kwa kutuunga mkono na kumfanya awe kama alivyo sasa," amesema Jembe.

## Prodyuza S2KIIZ atamba na BMW

MTAYARISHAJI wa muziki wa Bongo Fleva, S2KIIZ, amesema gari lake jipya aina ya BMW, amelinunua kutokana na mchango mkubwa wa Diamond Platnumz.

S2KIIZ, amesema yeye na Diamond, wametoka mbali na kila anachotaka kukifanya lazima amshirikishe ili kupata ushauri wake.

"Gari langu jipya limetokana na mchango mkubwa kutoka kwa Diamond, unajua yule jamaa huwa hakupatii pesa kama msaada, lakini malipo anayokupatia kutokana na kazi mnazozifanya unaweza kufanya jambo lolote linaloonekana kama hivi ninavyofanya," amesema S2KIIZ.

Kuanzia gari yangu ya kwanza hadi hii ya sasa amenisaidia kwa huwa akikupa malipo ya mara moja unaweza kufanya mambo makubwa.

Nimefanya kazi nyingi sana na Diamond, amenilipa pesa nyingi tunaandaa mawe makubwa sana itakuwa bora Afrika.




## Amigo achafua hali ya hewa

MWANAMUZIKI wa taarab, Prince Amigo, ameingia katika bifu na Mfalme wa muziki huo, Mzee Yusuph, baada ya kudai anatoa maneno mabaya dhidi yake kuwa analelewa na mwanamke.

Akizungumza katika kipindi cha Dadaz kinachorushwa na EATV, Amigo amesema yeye anamuheshimu na ndio maana hataki kumjibu licha ya maneno hayo kumuumiza roho yeye na familia yake.

Mzee Yusuph amenitukana sana, ananiambia eti mimi nalelewa na mwanamke, jambo hili nimelisikia na limeniuma sana lakini sikutaka kujibizana kwa sababu familia yangu imenikataza," amesema Prince Amigo.

Kuhusu suala la mke wake kufanya kazi katika bendi ya Mzee Yusuph, msanii huyo amesema hilo kwake halimpi tabu kwa sababu mwenyewe anajisimamia kwa kila kitu katika bendi yake.



HABARI MICHEZO

## Mourinho aiondoa Spurs katika mbio za ubingwa

**LONDON,** England

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Jose Mourinho, amesema licha ya ushindi mfululizo walioupata kwenye Ligi Kuu England, bado haoni nafasi ya wao kutwaa ubingwa.

Spurs imeanza msimu huu vizuri zaidi na leo Jumapili itacheza dhidi ya West Brom ikiwa haijafungwa kwenye Ligi Kuu tangu ilipochapwa na Everton.

Tottenham inaweza kupaa kileleni mwa msimamo kama watawafunga WBA, kabla ya Leicester City kucheza na Wolves na mabingwa Liverpool kuvaana na Manchester City.

Lakini Mourinho, ambaye ameshinda mataji matatu ya Ligi Kuu England kwa vipindi viwili alivyokaa pale Chelsea, ametupilia mbali uwezekano wa kutwaa ubingwa.

"Hapana, hapana, hapana," alisema Mourinho akiwaambia waandishi wa habari walipomuuliza kama anahisi Tottenham wapo kwenye nafasi ya kutwaa taji hilo msimu huu kwa mara ya kwanza tangu mwaka 1961.

"Nina uzoefu wa miaka mingi kwenye soka na ushindi wa mechi nyingi inanifanya nijisikie vizuri na sio kujiweka kwenye nafasi ya ushindi," amesema.





## MARTINEZ ANA IMANI KUMTUMIA LUKAKU

**BRUSSLES,** Ubelgiji

ROBERT Martinez anajiamini kwamba, Romelu Lukaku ataweza kuichezea Ubelgiji kwenye mechi zinazokuja, licha ya kuripotiwa kutokuwa fiti kwa straika huyo wa Inter Milan.

Lukaku alikaa benchi wakati Inter ikitoka sare ya 2-2 kwenye mchezo wa Ligi Kuu Italia, Serie A, na Parma na kufungwa 3-2 na Real Madrid kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kutokana na kuumia nyama za paja katika mchezo dhidi ya Shakhtar Donetsk.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 27 amekuwa akifuatiliwa kwa karibu na madaktari wa Inter na anaonekana anaweza kuukosa mchezo wa leo dhidi ya Atalanta.

Akizungumza mapema wiki hii, Mtendaji Mkuu wa Inter, Beppe Marotta amesema "akili ya kawaida" inatakiwa kutumika linapokuja suala la kuita wachezaji kwenye mechi za kimataifa.

Hata hivyo, Lukaku amejumuishwa kwenye kikosi cha Ubelgiji kwa mechi ya kirafiki dhidi ya Uswisi na ile ya Ligi ya Mataifa ya Uefa dhidi ya England na Denmark.

"Tumekuwa tukiwasiliana mara kwa mara na Inter," amesema Martinez katika mkutano wake na waandishi wa habari Ijumaa.

"Tunajiamini anaweza kuwapo Jumatatu. Anaweza kuwa tayari kwa kucheza."

## *Vinicius azungumzia shutuma Real Madrid*

**MADRID,** Hispania

VINICIUS Junior amesisitiza kushutumiwa ni jambo la kawaida kama unaichezea Real Madrid, ambapo ameielezea kama klabu bora zaidi duniani.

Nyota huyo wa kimataifa wa Brazil amekuwa na wakati mgumu wa kuwania namba kwenye kikosi cha kwanza pale Santiago Bernabeu tangu alipotua akitokea Flamengo mwaka 2018.

Amecheza mechi 53 za La-Liga tangu kuanza kwa msimu wa 2018-19 na 25 akiaanza huku akiwa amefunga mabao saba na kutengeneza moja.

Na hilo linamfanya nyota huyo mwenye umri wa miaka 20 kuwa na mchango mdogo wa mabao kuliko wenzake Marco Asensio (tisa), Lucas Vazquez na Isco (wote nane).

Na Vinicius amebainisha kwamba, kwa upande wake kupata shutuma ni jambo la kawaida, kwa sababu anacheza katika klabu kubwa.

"Mara zote nawafikiri wale wanaotaka ubora zaidi kutoka kwangu - familia, klabu, wachezaji wenzangu kama Marcelo na Casemiro, hao ndio wananiweka kwenye njia sahihi," amesema akiiambia Desimpedidos.

"Yote hayo ni kwa sababu ya mimi kuwa kwenye klabu kubwa duniani. Tunapopoteza mchezo wanazungumza kuhusu sisi, na tunaposhinda inakuwa ni kitu kingine tofauti kabisa."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# BARCA KUMWEKA MESSI NJIA PANDA

●●● Ni kutokana na uamuzi wa kumpunguzia mshahara endapo mshambuliaji huyo ataamua...

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA haitaweza kumudu kumbakiza Lionel Messi pale Camp Nou kwa mshahara wake wa sasa, kwa mujibu wa mgombea nafasi ya urais wa klabu hiyo, Toni Freixa.

**Mkataba wa Messi unatarajia kumalizika mwishoni mwa msimu huu na mfungaji huyo wa wakati wote wa klabu hiyo anaweza kuhitaji maboresho zaidi ya mkataba kama atabaki.**

Freixa amedokeza Barcelona haitaweza kumwongeza mshahara mshambuliaji huyo kwa sababu kiasi anacholipwa sasa ni kikubwa zaidi.

Lakini Freixa ana matumaini nyota huyo wa kimataifa wa Argentina ambaye ana umri wa miaka 33 ataweza kushawishika kubakia, licha ya Messi mwenyewe kutaka kuondoka kipindi cha majira ya joto.

Rais wa zamani wa klabu hiyo, Josep Maria Bartomeu, alionya kabla hajajiuzulu kwamba Barca itakumbwa na kushuka kwa mapato ya karibia euro milioni 300 kwa sababu ya mlipuko wa virusi vya corona.

Akizungumza na El Curubito, Freixa ameelezea matatizo ya kifedha yanayoikumba klabu hiyo.

Freixa alisema: "Tunazungumza kwa utulivu na leo, uso kwa uso na kuangalia namna gani Barca itaweza kumbakiza.

"Kwake yeye pamoja na wachezaji wote ambao watatakiwa kusaini mikataba mpya, tutatoa ofa inayowezekana kwa kila mchezaji."

Messi ni mchezaji ambaye analipwa mshahara mkubwa zaidi duniani kwa sasa akienda nyumbani euro 500,000 kwa wiki.

## ZISIKUPITE

### BARCA KUMUUZA DEMBELE

BARCELONA ipo tayari kuwauza wachezaji watano Januari, akiwamo anayewaniwa na Manchester United, Ousmane Dembele, 23. ***(Mundo Deportivo)***

### SKRINIAR ANUKIA LIVERPOOL

LIVERPOOL inawania kumsajili mlinzi wa Inter Milan, Milan Skriniar mwenye umri wa miaka 25, ili kuziba nafasi ya Virgil van Dijk ambaye ni majeruhi. Nyota huyo raia wa Slovakia anawaniwa pia na Tottenham.***(ESPN)***

### HAALAND NJIA MOJA

NYOTA anayewaniwa na Manchester United, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 20, ana makubaliano na Borussia Dortmund kuondoka klabuni hapo ifikapo mwaka 2022, lakini Real Madrid wana nafasi kubwa ya kumsajili straika huyo wa Norway. ***(AS)***

### NAGELSMANN ANUKIA UNITED

KOCHA wa RB Leipzig, Julian Nagelsmann, ameingia kwenye orodha ya makocha wanaowaniwa na Manchester United kwa ajili ya kuchukua nafasi ya Ole Gunnar Solskjaer. ***(ESPN)***

### POCHETTINO AIKATAA BARCA

KOCHA wa zamani wa Tottenham Hotspur, Mauricio Pochettino, amekataa mara mbili nafasi ya kuinoa Barcelona wakati akisubiria kuchukua mikoba pale Manchester United. ***(Star)***

### MOYES AMFUNDA SOLSKJAER

KOCHA wa zamani wa Manchester United, David Moyes, amemwambia Ole Gunnar Solskjaer kwamba, presha atakayopata pale Old Trafford ni kubwa kuliko sehemu nyingine yoyote katika soka. ***(Manchester Evening News)***

### CONTE AMFIKIRIA GIROUD

NYOTA wa Chelsea, Olivier Giroud mwenye miaka 34, Emerson Palmieri, 26 na Marcos Alonso, 29, bado wapo kwenye rada za kocha wa zamani wa Blues, Antonio Conte kule Inter Milan. ***(Football Italia)***

### ARSENAL YAMTAKA SZOBOSZLAI

ARSENAL inamwania kiungo wa Red Bull Salzburg na Timu ya Taifa ya Hungary, Dominik Szoboszlai, 20, kwa mujibu wa wakala wake. ***(Index)***

### SIMAKAN SOKONI

KLABU ya Marseille imejiondoa kwenye mbio za kuwania kumsajili mlinzi wa Strasbourg, Mohamed Simakan, 20, na pia anawindwa na Aston Villa. ***(Birmingham Mail)***

### PEARSON ATOA SIRI

KOCHA wa zamani wa Watford, Nigel Pearson amesema baadhi ya wachezaji wake walijua mapema kwamba anaondoka hapo kwenye klabu ya Vicarage Road kabla hajatimka. ***(Times)***

### CAMPBELL MTOTO AGOMBEWA

STRAIKA wa zamani wa Arsenal, Kevin Campbell amesema Celtic ilijaribu kumsajili mtoto wake, Tyrese, 20, wakati wa dirisha dogo la Januari, lakini kocha wa Stoke City anakocheza, Michael O'Neill alimshawishi kubaki klabuni hapo. ***(Football Insider)***

## HABARI MICHEZO

## Ngorongoro Heroes kibaruani leo

**Na Saada Akida**

TIMU ya Soka ya Taifa ya vijana wa umri chini ya miaka 20 (Ngorongoro Heroes), inatarajia kucheza mechi ya kirafiki ya kimaraifa dhidi ya yosso wenzao kutoka Sudan itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini, Dar es Salaam.

Ngorongoro Heroes na Sudan U-20 wanatarajia kutumia mechi hiyo na nyingine za kirafiki kwa ajili ya kujiandaa na mashindano ya vijana ya Afrika Mashariki na Kati yatakayofanyika kuanzia Novemba 20 hadi Desemba 10, mwaka huu jijini, Arusha.

Kocha Mkuu wa Ngorongoro Heroes, Jamhuri Kihwelo 'Julio', aliliambia gazeti hili kikosi chake kiko tayari kwa mchezo huo na anaamini watafanya vyema dhidi ya wageni wao Sudan.

Julio alisema amewaandaa wachezaji wake kucheza soka la utulivu na kutumia dakika za mapema kuwasoma wapinzani wao na baadaye wataongeza kasi kulingana na mfumo watakaoutumia. Alisema anatarajia kutoa nafasi kwa wachezaji wengi katika mechi hiyo ili kufahamu walivyoyapokea mafunzo yake.

Yosso wa Sudan waliwasili nchini tangu juzi, wakitokea jijini, Nairobi Kenya ambapo waliweka kambi ya muda mfupi. Baada ya mechi dhidi ya yosso hao wa Sudan, Ngorongoro Heroes inatarajiwa kusafiri kwenda Zanzibar ili kucheza michezo mingine dhidi ya wenyeji wao.

## Kiduku, Mthailand wasotea malipo

**Na Nelson Simon,** SAUT

KAMISHENI ya Ngumi za Kulipwa Tanzania (TPBRC), imewataka mapromota wa mchezo huo nchini kuwalipa mabondia stahili zao na kuacha tabia ya kukiuka mikataba waliyosaini kabla ya mapambano.

TPBRC imetoa tamko hilo baada ya kuwapo kwa malalamiko ya mabondia na waamuzi walioshiriki katika pambano lililofanyika hivi karibuni kwa kumshirikisha Twaha Kiduku na Sirimongkhon Lamthuam kutoka Thailand kutolipwa.

Akizungumza na jijini, Dar es Salaam , Kaimu Katibu Mkuu wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Neema Msitha, alisema kufanya hivyo ni kosa na serikali kama wasimamizi watawachukulia hatua mapromota wa mchezo huo.

"Kitu kilichoweza kufanyika ni kosa kubwa kwa waandaaji wa mchezo huo, walitakiwa kujipanga vyema katika kuwalipa fedha zao waamuzi na mabondia punde tu baada ya mchezo huo kumalizika," alisema Msitha.

Aliongeza BMT imejipanga kuweka sheria nzuri ili kuwaepusha mabondia kukutana na matatizo hayo katika siku zijazo.

Naye Kocha wa Twaha Kiduku, Charles Mbwana alisema bondia wake bado hajakabidhiwa fedha zake za ushindi na promota wa pambano hilo lililofanyika Oktoba 30, mwaka huu.

Kiduku anaendelea kujitengenezea rekodi nzuri katika mchezo huo baada ya kushinda mapambano 16, kupoteza sita na kupata sare moja.

# NDAYIRAGIJE ATAMBA KUWASHANGAZA TUNISIA

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI kikosi cha Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), kimeondoka nchini na kwenda kuweka kambi ya muda mfupi Uturuki, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Etienne Ndayiregije amesema wanaondoka wakiwa na lengo moja la kufanya vyema katika mchezo wao dhidi ya Tunisia utakaochezwa Novemba 13, mwaka huu jijini Tunis.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Ndayiragije alisema kuwa amewafuatilia wapinzani wao kwa muda mrefu na timu yake itaingia uwanjani ikifahamu ubora na upungufu ya wenyeji wao.**

Ndayiragije (pichani) alisema alikuwa na mawasiliano ya karibu na wachezaji wake wote aliowaita, hivyo maandalizi ya kuwakabili Tunisia ameyafanya kwa muda mrefu.



"Tunaondoka usiku wa kuamkia kesho (leo), tuko vizuri, tunaenda huko kwa kazi moja ya kupambana, naamini mechi itakuwa nzuri, ninawaandalia 'suprise'," Ndayiragije alisema kwa kifupi .

Kocha huyo aliongeza anahitaji kupata ushindi ili aweze kukaa kwenye nafasi nzuri katika kundi lao na kamwe haendi kutafuta matokeo mengine.

"Tunazihitaji pointi tatu, ndio maana ninasema tunakwenda kuwashangaza," aliongeza kocha huyo wa zamani wa Mbao FC, KMC FC na Azam FC zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara.

Aliongeza anaamini kila mchezaji aliyemwita atatoa mchango mkubwa kwenye timu kwa sababu wote 'wanasafiri njia moja' katika michuano hiyo.

Baada ya mechi hiyo ya kwanza, Taifa Stars inayoongozwa na nahodha, Mbwana Samatta, itarejea nchini mapema kwa ajili ya kuwakaribisha Waarabu hao katika mchezo wa marudiano utakaochezwa Novemba 17, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Katika mechi ya kwanza ya Kundi J, Stars ilikubali kichapo cha mabao 2-1 na Libya, mchezo ambao ulichezwa pia mjini Tunis.



Polisi wakimdhibiti 'komandoo' wa Yanga baada ya kufanya fujo kabla ya mchezo wa watani wa jadi, Yanga na Simba uliochezwa jana kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini, Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Mlandege, KVZ FC hapatoshi Z'bar*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MABINGWA wa Ligi Kuu Zanzibar, Mlandege FC, wanatarajia kukutana na KVZ katika mechi ya Ngao ya Jamii itakayofanyika leo kuanzia saa 10:00 jioni kwenye Uwanja wa Mau A, Visiwani hapa.

Mchezo huo ni maalumu kwa ajili ya kufungua msimu mpya wa Ligi Kuu Zanzibar mwaka 2020/21.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha wa KVZ, Sheha Khamis, alisema timu yake imejiandaa kupata ushindi katika mchezo huo ambao ni muhimu katika kufungua pazia la msimu mpya.

Sheha alisema kikosi chake kipo tayari na jana kilifanya maandalizi ya mwisho kuelekea mchezo huo ambao wanatarajia utakuwa na ushindani kutokana na kila upande kujipanga vyema.

"Kesho (leo), tumejiandaa kushindana licha ya kupata majeruhi wawili ambao walikuwa katika kikosi cha kwanza, hata hivyo hatufahamu rasmi kama tutawatumia au hatutowatumia maana tunasubiri ripoti ya mwisho wa daktari wetu," alisema Sheha.

Naye Kocha Mkuu wa Mlandege, Abdulhamid Rashid, alisema kikosi chake kimejiandaa vyema na kinaamini kitaibuka na ushindi licha ya kufahamu mpira ni mchezo wa mabadiliko.

"Tunafahamu wapinzani wetu wana kikosi chenye wachezaji wazuri na wenye uzoefu, lakini tunaamini kwa asilimia kubwa tutafanya vizuri, ingawa lolote linaweza kutokea ndani ya dakika 90," alisema kocha huyo.

Mlandege ndio wawakilishi wa Zanzibar katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika wakati mabingwa wa Kombe la FA, KVZ wao watapeperusha bendera ya Visiwa hivyo katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

# Michezo

Jumapili Novemba 8, 2020

Nipashe




Barca kumweka Messi njia panda UKURASA 22

# Yanga, Simba hakuna mbabe

## ●●● Onyango aiokoa Simba kupata kichapo, Tonombe...



Beki wa Simba, Shomary Kapombe (kushoto), akimtoka mshambuliaji wa Yanga, Ditram Nchimb, katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jana. Timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1. **PICHA: JUMANNE JUMA**

**Adam Fungamwango na**

**Saada Akida**

BAO lililofungwa na beki wa kimataifa kutoka Kenya, Joash Onyango dakika tano kabla ya pambano kumalizika, liliinusuru Simba na kipigo kutoka kwa Yanga katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyomalizika kwa sare ya bao 1-1 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini, Dar es Salaam jana.

**Kwenye mechi hiyo ya kiporo cha raundi ya saba kilichokuwa kichezwe Oktoba 18, mwaka huu Yanga iliongoza kwa muda mrefu kiasi cha mashabiki wengi kuamini Yanga ingetoka na pointi tatu kama ilivyokuwa Machi 8, mwaka huu kwenye mechi ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Bara msimu uliopita.**

Yanga ilianza mechi hiyo kwa kasi, huku Simba ikiwa imepooza. Wachezaji wa Yanga walionekana na kasi kubwa wanapoupata mpira nyuma na kusonga mbele, huku wa Simba wakicheza taratibu.

Kutokana na kasi yao kuwa kubwa, Tuisila Kisinda alikaribia kuifungia Yanga bao dakika ya 14 baada ya krosi kutoka kwa Michael Sarpong lakini shuti lake lilimbabatiza kipa wa Simba, Aishi Manula kifuani na baadaye kuudaka mpira huo.

Baada ya mashambulizi ya hapa na pale, Yanga ilipata bao la kwanza dakika ya 31 kwa njia ya penalti, baada ya Onyango kumwangusha kwa mikono Kisindа ndani ya eneo la hatari, ingawa picha za marudio zinaonyesha faulo ilikuwa nje ya eneo la 18. Alikuwa ni Sarpong aliyempeleka sokoni kipa Manula kwa kupiga upande wa kulia kwa kipa, huku yeye akiruka kushoto.

Almanusura Ditram Nchimbi aipatie Yanga bao la pili dakika ya 37 baada ya kuwazidi mbio mabeki wa Simba na kupiga shuti, ambalo kwa bahati mbaya kwake lilimbabatiza beki , Mohamed Hussein 'Zimbwe Jr' na kushindwa kutekeleza azma yake.

Kipindi chote cha kwanza, wachezaji wa Yanga walikuwa wakirudi nyuma wote kitu ambacho kiliwapa tabu wachezaji wa Simba waliokuwa wakicheza na straika mmoja tu, John Bocco.

Dakika ya 49, kipa wa Yanga Metacha Mnata aliiokoa timu yake isifungwe, baada ya kupangua mpira uliopigwa kichwa na nahodha wa Simba, Bocco.

Yanga, ambayo muda mrefu wa kipindi cha pili 'ilipaki basi' na kushambulia kwa nadra, nusura ipate bao la pili dakika ya 59, baada ya Mukoko Tonombe kuondoka na mpira na kuachia 'fataki' ambalo lingempa tabu Manula kudaka beki wake, Paschal Wawa asingeupiga kichwa na kuwa kona ambayo haikuzaa matunda.

Yanga ingeweza kutoka na ushindi kwenye mechi hiyo kama Farid Mussa angekuwa makini, kwani alikosa bao la wazi akiwa yeye na wavu baada ya kumegewa pande na Sarpong, lakini akiwa hatua mbili tu kutoka golini akapaisha na kuwashangaza waliokuwa uwanjani ambao waliamini anaipatia timu yake goli lingine.

Simba ambayo ilicharuka kipindi cha pili, itabidi ijilaumu yenyewe kwa kukosa mabao kupitia kwa Shomari Kapombe na Bocco ambaye dakika tatu kabla ya mechi kumalizika, aliunganisha krosi ya Kapombe, lakini mpira ukatoka nje kidogo ya lango.

Kwa matokeo hayo, timu hizo bado zimeendelea kufungiwa mabao na wachezaji wa kigeni kwenye mechi zao za 'dabi' za Ligi Kuu, kwani Sarpong ni raia wa Ghana na Onyango ni Mkenya.

Mghana Benard Morrison ndiye aliyeifungia Yanga bao pekee mechi ya mwisho ya Ligi Kuu timu hizo zilipokutana Machi 8, mwaka huu huku Simba mabao yao mara ya mwisho kwenye mechi za Ligi Kuu yalifungwa na Mnyarwanda Meddie Kagere na Mkongomani Deo Kanda, mechi iliyochezwa Januari 4 mwaka huu, ikiwa ni ya mzunguko wa kwanza wa ligi.

Hii inakuwa ni mechi ya nne kwa timu hizo kucheza mwaka huu wa 2020, tatu zikiwa ni za Ligi Kuu na moja ya Kombe la FA.

Timu hizo zimetoka sare mara mbili, na Yanga kushinda moja kwenye ligi, huku Simba ikishinda mechi moja kwenye Kombe la FA.

Kwa matokeo hayo, Yanga imeshindwa kuiondoa kileleni Azam, kwani imeokota pointi mmoja na kufikisha pointi 24 kwa mechi 10 ambazo imecheza, huku Azam ikiwa ina pointi 25 kwa mechi zake 10. Yanga bado inang'ang'ana kwenye nafasi ya pili, huku Simba nayo ikiota mizizi kwenye nafasi ya tatu kwa kufikisha pointi 10, nne nyuma ya Yanga na tano nyuma ya vinara Azam, timu zote tatu sasa zikiwa zimecheza mechi sawa.

Tonombe aliteuliwa kuwa mchezaji bora wa mechi hiyo na kupata zawadi ya Sh. milioni moja kutoka kwa benki ya KCB, ambao ni wadhamini washiriki wa Ligi Kuu Bara.

**'BABU' ONYANGO AFUNGUKA**

Huku akiibuka shujaa baada ya kuisawazishia timu yake bao, Onyango alisema ameonyesha umuhimu wake wa kusajiliwa kwenye kikosi hicho cha Msimbazi.

Onyango alisema amejisikia furaha kucheza katika dabi hiyo kwa mara ya kwanza na vile vile kuwa mfungaji wa bao muhimu.

"Pande zote zilikuwa na upinzani mzuri, wenzetu Yanga walikuwa na mchezo mzuri, naishukuru timu tangu kwa kupambana na hatimaye kupata pointi moja muhimu, tunashukuru," alisema Onyango.

Aliongeza malengo yao yalikuwa ni kupata ushindi, lakini wanalazimika kukubaliana na matokeo waliyopata kwenye mchezo huo.

"Mimi sina tatizo na hilo, kila mtu ana maneno yake anaweza kusema, mimi ninafurahia niko hapa, lakini wameona kile ambacho 'babu' amefanya, hata wakitaka kuniita nini, waniite, babu hawezi kuwafungа, lakini sasa amewafunga," Onyango alisema.

**MORRISON ASHANGILIWA**

Winga wa Simba, Bernard Morrison, alikuwa kivutio baada ya kuingia uwanjani na kuanza kuhamasisha mashabiki wa timu yake kushangilia kikosi chao kwenye mchezo huo wa mzunguko wa kwanza msimu huu.

Baada ya kuingia uwanjani, Morrison aliendа kukaa eneo la VIP na muda mwingi alihamasisha mashabiki kushangilia licha ya timu yao kuwa nyuma kwa bao moja kwa muda mrefu.

Katika pambano hilo ambalo Yanga walikuwa wenyeji, walitangulia kufika uwanjani na kufuatiwa na wapinzani wao, Simba dakika saba baadaye.

Hali ya mashabiki wa pande zote tangu wakiwa nje ya uwanja ilikuwa ya furaha na kujiamini, kuwa timu mojawapo itaondoka na ushindi katika pambano hilo.

Mzimu wa kugawana pointi kwa siku ya jana ulianzia kwa timu za vijana ambapo katika mechi ya mapema Yanga B ililazimishwa sare ya bila kufungana dhidi ya yosso wenzao wa Simba B.


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042